# Nipashe

Jumanne Februari 13, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581585

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11

**ZITTO** naye aitisha maandamano akilia na kero tatu kitaifa

UKURASA 4



**UTAPELI** mtandaoni bado tishio, laini 21,000 zafungwa

UKURASA 5

**ISRAEL** yashambulia usiku kucha, yaua watu wengi

UKURASA 19

# Kikwete: Lowassa nimeishi naye hivi

**ATINGA** na Mama Salma msibani; aweka sawa milima na mabonde yao... Uk. 2



Rais Mstaafu, Jakaya Kikwete, akisaini kitabu cha maombolezo nyumbani kwa marehemu Edward Lowassa, Masaki Dar es Salaam jana. Kulia ni mke wake, Salma Kikwete. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Dakika 25 zawapa tabasamu Papa, Rais Samia Vatican

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Papa Francis Vatican jana.

## Bunge laagiza mambo manane yasukwe upya Bima ya Afya

UKURASA 5

**MICHEZO** SIMBA YATETEMA MWANZA UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Kikwete: Niliishi na Lowassa hivi

**Na Waandishi Wetu**

RAIS mstaafu Jakaya Kikwete jana alifika kwenye msiba wa Waziri Mkuu wake wa kwanza, Edward Lowassa, akifunguka 'ya kabatini' maisha yao ya ofisini na uswahiba wao.

Lowassa aliyefariki dunia Jumamosi iliyopita, alikuwa sehemu ya safu iliyompambania Kikwete kwa mara ya kwanza katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1995 na ule wa 2005 uliomweka madarakani.

Kwa mujibu wa Kikwete, Lowassa ni sehemu ya 'mabwana mipango' watatu waliomshawishi kuwania nafasi ya wadhifa ambao leo unampa hadhi Rais mstaafu.

"Ninamfahamu marehemu (Lowassa) kwa muda mrefu, tulikuwa vijana pamoja, tulikuwa chuo kikuu (UDSM) pamoja, nilimtangulia mimi mwaka mmoja," alitamka Kikwete kwa sauti ya utashi, akiendelea:

"Tulitangulia sisi kuingia kwenye chama (TANU) na baadaye yeye akafuata. Tumefanya kazi wote kwenye chama kwa muda wote, mimi nikaendelea na shughuli za jeshi (JWTZ) na baadaye tena nikarudi kwenye chama.

"Mwenzangu aliendelea moja kwa moja kwenye shughuli za chama, baadaye akawa mbunge na mimi baadaye nikateuliwa kuwa mbunge, naibu waziri. Kwa hiyo, tukawa wote kwenye harakati za kisiasa."

Akiwa ameambatana na mkewe, Salma, Kikwete pia alizungumzia misukosuko ya kisiasa iliyowagusa katika urafiki wao, akiitaja kuwa "ni changamoto kwenye maisha na haifuti mema na mazuri aliyolifanyia taifa".

Lowassa alitumikia nafasi ya Waziri Mkuu katika zama za Kikwete kwa miaka miwili na miezi kadhaa kabla ya kujiuzulu na baadaye kuibukia kuwa mgombea urais kwa tiketi ya CHADEMA baada ya kukwama kuipata tiketi hiyo kwa kofia ya CCM mwaka 2015.

Kikwete alisimulia mkasa wa mwaka 1995, akiwa nyumbani kwake, alifuatwa na marafiki zake watatu wakiongozwa na aliyewahi kuwa Spika wa Bunge, Hayati Samuel Sitta, Lowassa na Rostam Aziz. Wakamshauri aende na rafiki yake (Lowassa) kuchukua fomu ya kuwania urais.

"Mwaka 1995, siku moja asubuhi, nikapokea ugeni, mtoto akaja chumbani, akaniambia 'baba kuna wageni'. Nikaenda chini nikakuta marafiki zangu watatu, kaka yangu Samwel Sitta, Edward Lowassa na Rostam Aziz. Wakaja kuniambia kwamba 'tunataka mwende na Edward Dodoma mkachukue fomu.

"Mimi nikasema 'jambo hilo halipo kwenye mawazo yangu', lakini mwenzangu lipo kwenye mawazo yake... nikasema 'basi mwacheni aende...' naye akasema 'na mimi siendi bila wewe'. Basi ikabaki ndiyo historia.

"Tukabishana mpaka tukafika mahali tukakubaliana... 'basi wacha twende'. Kwahiyo, tukaenda tukachukua fomu zile tukazijaza, zikarudishwa... mchakato ndani ya chama... mwenzangu hakubahatika... mimi nikabahatika kuwamo katika wale watano.

"Na baadaye tukapigiwa kura kwenye NEC nikawamo kwenye wale watatu... kwenda mkutano mkuu... nikawamo katika wawili na tulivyobaki wawili kura zangu hazikutosha... akapata Mzee Mkapa... mimi nikaja kuwa Waziri wake wa Mambo ya Nje na mwenzangu (Lowassa) akaja kuwa waziri tena," alisimulia.

Kikwete alisema wakiwa wanatumikia nafasi hizo, waliendelea kuweka mikakati kwa ajili ya kugombea tena katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005.

"Basi tumeendelea hivyo na kuweka mikakati ya pamoja ya mwaka 2005, tukateuliwa kugombea, mwenzangu akateuliwa kuwa Waziri Mkuu... akapata changamoto katikati, ikabidi akae pembeni... lakini tukaendelea kuwa pamoja, kuwa marafiki, tukishirikiana kwa kila linalowezekana.

"Ameugua, Mwenyezi Mungu ameichukua roho yake. Ninachoshauri tu tuendelee kumwombea, (Mungu) aipokee roho yake na aiweke mahala pema peponi.

"Edward ametoa mchango mkubwa kwa taifa letu, yaliyotokea ni changamoto katika maisha, lakini hayafuti yale mema na mazuri aliyolifanyia taifa letu," alisema.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi alisema amepokea taarifa za kifo cha Lowassa kwa masikitiko makubwa kwa sababu walifanya naye kazi wakiwa mawaziri katika serikali ya awamu ya tatu.

Alisema amekwenda kutoa salamu za pole kwa familia ya marehemu kwa niaba ya wananchi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutambua mchango mkubwa wa kiongozi huyo kwa taifa.



Mwenyekiti wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere Joseph Butiku, akisaini kitabu cha maombolezo kwenye msiba wa Edward Lowassa, Masaki, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI**

**WATAKA KITABU**

Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Khenani na Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, wameomba kiandikwe kitabu cha kumbukumbu ya Lowassa ili kumbukumbu nzuri kuhusu maisha yake ya uongozi na siasa zibaki kuwa funzo kwa viongozi na wanasiasa wengine nchini.

Wanasiasa hao walitoa kauli hiyo kwa nyakati tofauti wakati wakizungumzia milima na mabonde aliyopitia Lowassa.

Zitto alisema kitendo cha Lowassa kujiuzulu nafasi yake lilikuwa ni jambo kubwa ambalo linapaswa kuwa mfano kwa viongozi wengine pale inapowabidi kufanya hivyo.

"Lowassa alipata ajali ya kisiasa, ikatokea skendo kubwa tu ya Richmond, Kamati ya Bunge ikatoa taarifa na mimi nilikuwa bungeni siku ile, na yeye akaona kwamba ametajwa, na alisema siku ile kwamba 'nimeonewa na sikupewa nafasi ya kusikilizwa, lakini inaonekana shida ni Waziri Mkuu', akaachia nafasi hiyo.

"Ni hatua kubwa sana kwa sababu Waziri Mkuu, katika nchi yetu ni mtu wa tatu katika utendaji na uongozaji wa serikali na dola, na alikuwa mtu wa kwanza kuzungumza bungeni siku ile, na akamaliza mjadala kwa kujiuzulu na serikali nzima ikaanguka, Rais Kikwete akatafuta Waziri Mkuu mwingine, akaunda serikali," alisema Zitto.

Alisema licha ya Lowassa kuanguka kisiasa, baadaye aliibuka na kuwa mwanasiasa mkubwa na kila mtu akawa anataka kumwona na kuwa upande wake. Kumbukumbu hizo zote zinapaswa kuwekwa kwenye vitabu ili kubaki kuwa funzo.

"Ingekuwa ni nchi nyingine sasa hivi kungekuwa kuna vitabu kuhusiana na kuanguka na kusimama kwa Lowassa, lakini nchi yetu utamaduni ni mdogo, kulipaswa kuwa na utafiti wa kutazama hayo.

"Maana yake ninakumbuka mwaka 2008, Lowassa alikuwa akitembea anaweza kuzomewa, lakini miaka miwili baadaye kila mtu alitaka kuonana naye, kila mtu alitaka kuwa upande wake," alisema.

Zitto alikumbushia pia 'Safari ya Matumaini' aliyoianzisha Lowassa na namna 'ilivyosomba' watu.

"Kama kuna jambo ambalo ninaweza kujifunza kwa Lowassa ni uwezo wa kufanya uamuzi, lakini neno lingine kwa taifa na kwa Rais wa Jamhuri, lazima tufanye kitu cha kumthamini na kumkumbuka Lowassa," alisema.

Mbunge Khenani (CHADEMA) alisema Lowassa alionesha mfano wa kuigwa kwa kutanguliza maslahi ya taifa badala ya maslahi yake pale alipoonesha uthubutu na kujiuzulu.

"Kwenye uongozi ameacha alama yake, kama kiongozi lazima uoneshe mfano wa kuigwa, alionesha pamoja na kwamba alikuwa na nafasi kubwa ya Waziri Mkuu, akajiuzulu.

"Kwa wale ambao wanaweza kusaidia hasa familia yake, yale wanayoyajua na watu wa karibu wasaidie kuacha kumbukumbu halisi kwenye taifa letu kwa sababu wana alama yake," alisema mbunge huyo akikumbuka pia mchango wa Lowassa kwa CHADEMA kuchukua viti vingi vya ubunge na udiwani mwaka 2015.

**STEVEN WASSIRA**

Mwanasiasa mkongwe, Stephen Wassira alisema Lowassa alifanya kazi kubwa ndani ya CCM na serikali. Katika awamu ya tatu aliimarisha utoaji elimumsingi.

"Ninachoweza kuongea ni kwamba msiba wa ndugu yetu Edward Lowassa umetuondolea mtu muhimu sana ambaye alikuwa anatoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya nchi yetu," alisema.

Aliwasihi Watanzania kuwa wakati wanaombeleza kifo cha kiongozi huyo wasikubali msiba wake uwagawe kichama au kitaifa, bali uwe kiungo cha kuwaunganisha na kuwafanya kuwa wamoja.

Mfanyabiashara Azim Dewji alisema Lowassa alikuwa kiongozi mwenye uchungu na nchi yake na kutaka watu wote wafahamu kuwa nchi ni yao na kufanya kazi kwa maslahi ya nchi.

**PAUL MAKONDA**

Katibu wa NEC (CCM) Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Paul Makonda, alisema alichojifunza kwa Lowassa ni ustahamilivu kwa kuwa katika maisha yake hajawahi kuinua kinywa chake na kujibu mapigo katika mapambano yote aliyoyapitia.

Aliwasihi Watanzania kumwenzi kiongozi huyo kwa kuiga mfano wa mema aliyoyatenda ikiwamo kutowekeana uhasama na visasi, bali washikamane na kujenga nchi.

Makonda pia aliwataka watu kuacha kumzungumzia mtu kwa mazuri pale anapofariki dunia, akisisitiza wale ambao hawakwenda kumjulia hali wakati anaumwa, waache alichokiita unafiki kwa kujifanya kuwa ni rafiki yao.

"Tuache unafiki kuna wengine wanajiita marafiki wa Lowassa na hawakwenda kumwona halafu baada ya kufariki dunia wanajifanya wao marafiki zake, lakini hawakujitokeza, waache kumsemea mtu mazuri baada ya kufa," alisema.

INAENDELEA UK. 3

# Kikwete: Niliishi na Lowassa hivi

INATOKA UK. 2

**SHEIKH MKUU**

Sheikh Mkuu wa Tanzania, Dk. Abubakar Zubeir, aliwasihi wananchi kuendelea kumkumbuka kiongozi huyo kwa mazuri aliyoyafanya kwa taifa.

Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, akizungumzia maisha ya kisiasa ndani na nje ya CCM na utendaji wa Lowassa, alisema hakuwa kiongozi aliyekuwa anasema 'nenda uje kesho'.

**LUHAGA MPINA**

Mbunge wa Kisesa, Luhaga Mpina, pia alimwelezea Lowassa kama Waziri Mkuu aliyekuwa na uamuzi mgumu, akitilia mkazo kuimarisha sekta ya elimu.

"Taifa limepata hasara kubwa ya kumpoteza aliyekuwa Waziri Mkuu, Edward Lowassa. Kwa kweli tutamkumbuka kwa mambo mengi. Moja ni uwezo mkubwa wa Lowassa katika kusimamia shughuli za serikali.

"Kile kilichopangwa kufanyika alikuwa na uwezo mkubwa sana wa kukisimamia na kukifuatilia. Wote mtakumbuka wakati tunaanza ujenzi wa shule za sekondari kila kata mwaka 2006, Lowassa akiwa Waziri Mkuu, alituita viongozi wa maeneo mbalimbali na kupewa maelekezo kwamba tunaanza ujenzi wa shule za kata na alisimamia hilo," alisema

**NAIBU SPIKA**

Mussa Zungu, Naibu Spika alisema Lowassa alikuwa na uamuzi mgumu na alikuwa mkali, mcheshi na hakupenda kumwonea mtu wala kumdharau mtu.

Alisema wakati yeye akiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Lowassa alikuwa Mwenyekiti wake, ndiko alikoanza kumjua vizuri, akaona uwezo, nguvu zake na ushawishi wake kwa mabalozi wa nchi mbalimbali.

"Huu ni msiba mkubwa sana kwa Watanzania wote. Mimi binafsi nimeguswa sana na msiba huu. Niliwahi kukutana na Lowassa katika zaira yake Mkoa wa Dar es Salaam, alivyokuja na ajenda za shule za kata, na yeye kipindi kile alikuwa na Waziri Mkuu na Waziri wa Elimu alikuwa Magreth Sitta. "Niliona namna alivyohangaikia shule zile, na kwa kweli shule hizi, ndio sasa zilizofaulisha watoto wetu, na vijana wengi wanapata division One (daraja la kwanza) kutoka shule zile," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Dar es Salaam, Mariam Kisangi, alisema Lowassa atakumbukwa kwa kuacha alama ya kudumu katika sekta ya elimu nchini, hasa pale alipotafuta mwarobaini wa changamoto kubwa ya watoto waliofaulu darasa la saba kukosa madarasa ya kusomea kidato cha kwanza.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka alisema Lowassa alikuwa mwanasiasa na kiongozi mwenye kishindo.

"Ninaweza kusema ulikuwa tembo wa siasa za CCM, kwa kauli na matendo ulibeba haiba ya kiongozi mwenye maono, matamanio na uamuzi wenye matokeo. Alama ya kazi zako kwa taifa lako pendwa la Tanzania hazihitaji tochi," alisema.

**-Imeandikwa na Elizabeth Zaya na Jenifer Gilla (DAR), Godfrey Mushi (DODOMA)**



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akisalimiana na Naibu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Changamoto za Milenia, Chidi Blyeden, walipokutana na kufanya mazungumzo na ujumbe wa shirika hilo kuhusu namna Tanzania itakavyotekeleza na kunufaika na mpango wa ruzuku zinazolenga kusaidia mageuzi ya kisera na kitaasisi ili kutatua vikwazo vya ukuaji uchumi mazungumzo hayo yalifanyika katika Ofisi za Hazina Ndogo, jijini Dar es Salaam jana. **Habari Uk 5**. **PICHA: WIZARA YA FEDHA**

# Dakika 25 zawapa tabasamu Papa, Rais Samia Vatican

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameteta na Papa Fransisco jijini Vatican katika mazungumzo ya faragha yaliyodumu kwa dakika 25, baadaye kuripotiwa wameridhika na uhusiano wa kidiplomasia kati ya Vatican na Tanzania.

Radio Vatican ndiyo iliyoripoti mazungumzo hayo ya faragha, ikieleza kuwa viongozi hao pia wameridhika na mchango wa Kanisa Katoliki katika ustawi na maendeleo ya watu wa Mungu husan katika sekta za elimu, afya na ustawi wa jamii.

"Baadaye wamejielekeza zaidi katika masuala ya kijamii, kikanda na kimataifa na umuhimu amani," aliripoti Padri Richard Mjigwa akiwa Vatican.

Taarifa zinaonesha kwamba ni miaka 12 tangu Rais wa Tanzania azuru Vatican. Rais mstaafu Jakaya Kikwete alimtembelea Papa Benedikto XVI Januari 19, 2012 na kuzungumza naye kwa dakika 15.

Akizungumzia uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na Vatican, Padre Mjigwa alisema ulianzishwa Aprili 19, 1968 na kwamba Askofu Mkuu Pierluigi Sartorelli, aliteuliwa kuwa Balozi wa kwanza wa Vatican nchini, nafasi aliyoitumikia hadi Desemba 22, 1970.

"Uhusiano huu kama alivyobainisha Baba Mtakatifu Benedikto XVI wakati akipokea hati za utambulisho kutoka kwa Balozi Ali Abeid Aman Karume wa Tanzania mjini Vatican, unasimikwa katika tunu msingi za amani, haki, mshikamano na uhuru, kwani haya ni mambo yanayopata asili yake kutoka katika utu, heshima na haki za msingi za binadamu, ustawi, maendeleo na mafao ya wengi yakipewa msukumo wa pekee," alifafanua.

Baada ya kuzungumza na Papa Fransisco, Rais Samia alikutana na kuzungumza na Kardinali Pietro Parolin, Katibu Mkuu wa Vatican aliyekuwa ameambatana na Askofu Mkuu Paul Richard Gallagher na Katibu Mkuu wa Mambo ya Nchi za Nje, Ushirikiano na Mashirika ya Kimataifa.

Padre Mjigwa alisema Kanisa Katoliki Tanzania limekuwa mstari wa mbele katika kuchangia ustawi na maendeleo ya wananchi kupitia elimu, afya, maendeleo na ustawi wa jamii na huduma ya maisha ya kiroho.

Kwa mujibu wa Padre Mjigwa, Kanisa Katoliki nchini linamiliki na kuendesha shule za awali 240, za msingi 147, sekondari 244, vyuo vya ufundi na vyuo vikuu vitano.

"Shule na taasisi za elimu ya juu pamoja na vyuo vikuu vinavyomilikiwa na kuendeshwa na Kanisa Katoliki, vimekuwa ni vituo makini vya kuandaa vijana kiakili, kimaadili, kiroho na kiutu kwa kuzingatia ubora na viwango vya kitaifa na kimataifa," alisema.

Katika mkutano wa Januari 19, 2012, Rais mstaafu Kikwete na Papa Benedikto XVI waligusia majadiliano ya kidini na amani katika eneo la Maziwa Makuu, afya, ustawi, maendeleo na maslahi ya wengi.

Katika ziara yake, Rais Samia ameambatana na Mama Evaline Malisa Ntenga, ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya Umoja wa Wanawake Wakatoliki Duniani na Rais wa Umoja wa Mashirika ya Kikatoliki Duniani (WUCWO) barani Afrika, ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Wakatoliki nchini (WAWATA).

Pia ameambatana na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Walei Taifa, Prof. Deogratias Rutatora, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana Wakatoliki Wafanyakazi Tanzania, Leonard Mapolu, Mwenyekiti wa Halmashauri Walei, Jimbo Katoliki la Zanzibar, Dalmas Gregory na Mwenyekiti wa Utoto Mtakatifu, Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Theresia Seda.

Wengine ni baadhi ya viongozi waandamizi serikalini akiwamo Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba.




Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramdhan Soraga (katikati), akiwa pamoja Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe Juma (wa pili kushoto), Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Oryx Gas, Benoite Araman (kushoto) na Katibu wa Idara ya SUKI CCM, Zanzibar, Khadija Salim (wa pili kulia), wakimkabidhi mtungi wa gesi ya kupikia ya ORYX mmoja wa wajasiriamali, mitungi 1000 ilikabidhiwa jana katika viwanja vya Maisara, Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zitto naye aitisha maandamano

**Na Maulid Mmbaga**

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, ametaja masuala matatu ambayo ameonya kuwa yasipofanyiwa kazi, yatasababisha madhara kwa taifa.

Amesema moja ya mambo hayo ni uhaba wa ajira kwa vijana, akiutaja ni "mwiba mchungu kwa taifa", lakini serikali haijielekezi kisera kujenga uchumi unaozalisha ajira nyingi, bora na zenye staha.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam wakati wa kikao cha wajumbe wa Halmashauri Kuu ya chama hicho, Zitto alitaja changamoto nyingine ni migogoro ya ardhi na ya mipaka kati ya hifadhi na vijiji pamoja na kupanda kwa gharama za maisha kunakosababisha wananchi kushindwa kumudu maisha ya kila siku.

Zitto pia alisema wamesikitishwa na kusuasua kwa miradi miwili ukiwamo wa kuchakata gesi asilia wa Lindi na wa kuzalisha chuma na makaa ya mawe ulioko Mkoa wa Njombe, akieleza kuwa ina faida kubwa kwa uchumi na ina fungamanisho imara kwa sekta nyingi za uchumi.

"Wakati mwingine huwa ninawaza kwamba labda kuna uchawi katika uendeshaji wa serikali, ambao unawafanya viongozi wenye dhamana kuachana na mambo ya maana ambayo faida yake haimithiliki," alisema Zitto.

Aliongeza kuwa endapo mradi wa gesi (LNG) Lindi wenye thamani ya Dola bilioni 40, mkataba wake ungetiwa saini tangu mwezi Mei 2023, ungeongeza ajira katika mnyororo wa thamani pamoja na mapato ya fedha za kigeni na kuwafanya wasihangaike na ukosefu wa dola unaolalamikiwa kwa sasa.

Alitoa rai kwa serikali iache kusuasua katika mambo yenye kila dalili za kuibadilisha nchi kiuchumi.

Alisema ni jambo la kushangaza kuagiza chuma kutoka nje cha thamani ya Dola bilioni moja kila mwaka, ilhali Ludewa kuna chuma kimelala miaka zaidi ya 1,000 kwenye mradi wa Mchuchuma na Liganga.

"Serikali itambue kwamba vijana wa Tanzania wamechoka kusikia masimulizi na sababu zilezile kila siku. Watanzania wanataka kuona uamuzi ukichukuliwa ili ajira nyingi na bora zitengenezwe na taifa lipige hatua kubwa.

"Tunaitaka serikali iweke wazi ratiba ya utekelezaji miradi hii muhimu sana kwa uchumi wa taifa. Niwatake viongozi wetu wa mikoa ya Lindi na Njombe na wilaya zake mtakaporudi kwenye mikoa yenu mfanye mazungumzo na wanachama na wananchi wa mikoa hii kupata njia za kushinikiza miradi hii kuanza kutekelezwa.

"Ikiwezekana hata kufanya maandamano ya amani ya mara kwa mara kwenye mikoa yenu kushinikiza miradi hii kuanza ili kuzalisha ajira kwa vijana wetu, kukuza uchumi wetu na kuongeza mapato ya fedha za kigeni kwa taifa letu.

"Tusiruhusu warasimu wachache serikalini kwa sababu wanazojua wao kuchelewesha miradi muhimu na ya kimkakati," alisema Zitto.

Alitoa rai kwa viongozi na wanachama wa chama hicho kuimarisha umoja na mshikamano kwa maslahi mapana ya chama hicho na wananchi kwa ujumla, akisisitiza kuwa kukitokea mjumbe atakayewasilisha hoja ya kuwatenga kama chama, 'wambwage'.

Vilevile, alisema utamaduni wa uongozi wa pamoja unataka kufanya uamuzi wa kitaasisi kupitia maboresho ya katiba yao.

Alisisitiza kila mwanachama na kiongozi wa ACT afahamu kuwa kwenye chama hicho anapewa dhamana na wenzake kulingana na mahitaji ya wakati huo.

"Ikifika wakati mwanachama mwingine anapaswa kubeba dhamana, haina maana kuwa aliyekuwapo kashindwa, la hasha! Bali mazingira yanataka ili kufikia malengo yetu na shabaha, mwanachama mwingine abebe maono na wengine tumsaidie kumwondolea magugu kwenye njia ili atufikishe," alisema Zitto.

Aliongeza: "Kila mmoja wetu ana wajibu wa kusimama pamoja kama timu moja, tukiwa na lengo moja la kufanikisha malengo na mipango ya chama chetu.

"Tulinde na kuimarisha umoja wetu, tukijua kwamba nguvu zetu zinapatikana katika umoja wetu. Tuweke kando tofauti zetu za kibinafsi na tuzingatie maslahi ya pamoja ya chama chetu," alisisitiza Zitto.

# Apandishwa kizimbani kwa mashtaka ya kunajisi mtoto

**Na Samson Chacha,** TARIME

MKAZI wa Kitongoji cha Sang'ang'a, Kijiji cha Nyabisaga, Kata ya Pemba, wilayani Tarime, Kassim Matiko (42) amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Tarime, akikabiliwa na mashtaka ya kunajisi mwanafunzi wa darasa la saba wa Shule ya Msingi Sang'ang'a.

Imedaiwa mahakamani kuwa mshtakiwa kwa nyakati tofauti alitenda ukatili dhidi ya mtoto huyo (jina tunalo) wakati mtoto huyo alipokwenda kuchota maji kwenye kisima cha mshtakiwa.

Akisoma mashtaka hayo mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Tarime, Stanley Mwakihaba, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Davis Kasesigwa alidai mshtakiwa alinajisi mwanafunzi huyo kwa nyakati tofauti kati ya tarehe 29 Desemba 2023 na 31 Desemba 2023 wakati mwanafunzi huyo alipokwenda kuchota maji mchana kwenye kisima hicho.

Mtuhumiwa Kassim alikana kutenda Kosa hilo na kuomba dhamana. Hakimu Mwakihaba alitoa masharti ya dhamana kuwa na wadhamini wawili, kila mmoja awe mtumishi wa umma na aweke bondi ya Sh. milioni tano.

Mshtakiwa alishindwa kutimiza masharti ya dhamana, hivyo kupelekwa mahabusu hadi tarehe 20 Februari mwaka huu kesi yake ikatajwa tena kwa ajili ya kusomewa maelezo ya awali kuhusiana na mashtaka yanayomkabili.

# Matumizi ya P2 yazua jambo bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MATUMIZI holela ya njia ya dharura ya vidonge vya uzazi wa mpango (P2) yameibuliwa tena bungeni, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Thea Ntara akitaka serikali kuja na utaratibu wa kudhibiti matumizi hayo hasa kwa mabinti kwa kuwa kuna hatari wasipate watoto pindi watakapokuwa tayari kuzaa.

Akiuliza maswali bungeni jana, mbunge huyo alisema matumizi ya P2 yamekuwa tishio kwa mabinti, wanatumia dawa hizo kama wanavyotumia dawa za kupunguza maumivu.

"Yaani hakuna utaratibu, tutafika wakati mabinti watashindwa kupata watoto. Je, serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa mabinti ili kuacha matumizi ya P2 na vinywaji vya kuongeza nguvu?" alihoji.

Mbunge wa Kinondoni (CCM), Abbas Tarimba, alihoji sababu za serikali kutoa rukhsa ya dawa aina ya P2 kutumika licha ya kukiri kuwa na madhara.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema matumizi ya ovyo ya P2 yanasababisha madhara mengi ikiwamo kupata matatizo ya mifupa.

Aliomba wabunge kuendelea kuhamasisha matumizi sahihi ya P2 kwa kuzingatia ushauri wa kitaalamu.

"Suala la Sayana Press na Depo ni dawa za aina moja, unachomwa kwenye misuli na hii nyingine unachomwa kwenye ngozi, Sayana Press ikiruhusiwa ovyo ovyo, tutaingia kwenye matatizo sawa na P2," alisema.

Katika majibu yake kwa swali la Mbunge Tarimba, Dk. Mollel alisema dawa yoyote isipotumika kwa kufuata taratibu ina madhara na kwamba shida iliyoko kwenye P2 ni kutumia kila wakati kinyume cha taratibu.

"Unafanya haya mambo bila kufuata utaratibu halafu unameza P2, haya ndio yanayotuletea shida. Tunataka watu wafuate taratibu zinazotakiwa," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge Ntara alihoji mpango wa serikali kutoa rukhsa kwa kutumika Sayana Press kama njia ya uzazi wa mpango badala ya kutumia P2 bila utaratibu.

Naibu Waziri Mollel, akijibu swali hilo, alisema Sayana Press imesajiliwa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) na inapatikana kwenye vituo binafsi vya kutolea huduma za afya kwa wateja wanaohitaji.

"P2 ni njia ya dharura ya vidonge vya uzazi wa mpango ambayo hutumika kuzuia mimba kwa mwanamke aliyefanya tendo la ndoa bila kinga.

"Kwa mfano, aliyebakwa au ametumia mpira wa kiume ukapasuka na anadhani anaweza kupata mimba asiyoitarajia wakati Sayana Press ni njia ya kuzuia kupata ujauzito kwa muda mrefu, hivyo matumizi ya kuzuia mimba kwa Sayana Press na P2 ni tofauti," alifafanua.

# Bunge laagiza kufumua sheria iliyoanzisha NHIF

Na Godfrey Mushi, DODOMA

BUNGE limeagiza kufanyika mambo manane ili kushughulikia changamoto za uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), likiitaka serikali ianze mchakato wa kurekebisha sheria ya mfuko huo.

Chombo hicho pia kimeagiza kitita cha bei kinachotumika sasa kiendelee kutumika katika kipindi cha mpito hadi pale kitita kipya cha bei kitakapozingatia maoni ya wadau wote wa sekta ya afya ya umma na binafsi.

Vilevile, Bunge limeagiza serikali ianzishe chombo huru mahususi na cha kudumu kitakachoratibu na kusimamia bei za huduma za afya ambacho kitajumuisha wajumbe kutoka sekta ya umma na sekta binafsi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya Ukimwi, Stanslaus Nyongo, alisema jana kuwa imebainika kuwapo upungufu katika sheria iliyoanzisha NHIF, hivyo Bunge linaazima serikali ianzishe mchakato wa kurekebisha sheria hiyo ili kuitambua sekta binafsi ya afya.

Nyongo ambaye ni Mbunge wa Maswa Mashariki, alikuwa anawasilisha bungeni jijini Dodoma taarifa ya shughuli za kamati hiyo kwa mwaka 2023.

"Bunge linaazimia Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) iwezeshwe kisheria kwa kuwekewa kanuni chini ya Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ili kuipa mamlaka ya kudhibiti utoaji huduma za bima ya afya nchini.

"Vituo vya afya binafsi viruhusiwe kuwa na utaratibu wa mgonjwa kuchangia huduma (co-payment), ambapo wamiliki wa kadi za NHIF watatakiwa kulipa kwa fedha taslimu gharama zinazozidi kiwango cha kitita kinachochangiwa na NHIF.

"Na NHIF ianzishe kamati ya wataalamu ambao watakuwa wanapitia malalamiko ya kitaaluma yanayowasilishwa na vituo vya kutolea huduma au wataalamu kuhusu bima ya afya," alisema.

Wakati anatoa taarifa hiyo, Nyongo alisema Bunge linaazimia pia serikali ikamilishe mchakato wa kufanya tathmini ya vyanzo na viwango vya fedha kwa ajili ya mfuko wa kugharamia bima ya afya kwa watu wasiokuwa na uwezo kupitia Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

Kuhusu uwiano wa upatikanaji huduma za vitita vya bima ya afya, mwenyekiti huyo alilieleza Bunge kuwa kifungu cha 15(2) cha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kinataka mtu yeyote awe na angalau kitita cha bima ya afya ya jamii.

Alisema katika hali halisi, mbali na watu wasiokuwa na uwezo wanaotakiwa kusaidiwa na serikali, watu wenye uwezo wa chini watajikuta wanalazimika kuwa na kitita hicho.

Akisisitiza kundi hilo lina idadi kubwa ya watu, hivyo huduma wanayoweza kupata kwa utaratibu wa sheria hiyo inapaswa kuangaliwa vizuri. Ili kugharamia bima kwa watu wasio na uwezo, serikali imepanga kutumia vyanzo mbalimbali ikiwamo fedha zinazokusanywa kutoka chanzo cha miamala ya kielektroniki na kuongeza asilimia mbili ya ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa za vinywaji vyenye kaboni.

Vimo vyanzo kama kuongeza asilimia mbili ya ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa za vinywaji vikali na kuongeza asilimia tatu ya ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa za vipodozi.

Vilevile, serikali imepanga kuongeza asilimia mbili ya kodi inayotozwa kwenye michezo ya kubahatisha na kuongeza asilimia tano kwenye ada ya bima za vyombo vya moto.

Vyanzo hivyo vitawezesha mapato ya Sh. bilioni 273.25 kwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji. Kwa makadirio ya serikali, mahitaji katika kipindi hicho ni Sh. bilioni 266.96.



Ofisa Mpima Ardhi wa Mkoa wa Songwe, Bernado Nkuwi, akionesha Mto Runzenga ambao ni mpaka kati ya Songwe na Mbeya jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TCRA yafungia laini 21,000 zilizohusika kwenye utapeli

Na Mwandishi Wetu

ZAIDI ya laini 21,788 za mawasiliano ya simu zimefungiwa kupokea na kutoa mawasiliano kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kutumika kufanya uhalifu mtandaoni kwa kipindi cha miezi mitatu iliopita.

Kwa mujibu wa ripoti ya mwenendo wa sekta ya mawasiliano iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Jabiri Bakari jana, idadi ya matukio ya ulaghai imeendelea kupungua kutoka laini za simu 23,328 zilizofungiwa Julai na Septemba 2023 hadi laini za simu 21,788 kwa Oktoba hadi Desemba 2023 ikiwa ni upungufu wa laini za simu 1,540, sawa na asilimia 6.6.

Aliitaja mikoa inayoongoza kwa matukio ya simu za ulaghai hadi kufikia Desemba mwaka 2023 na idadi ya kwenye mabano ni Rukwa (7,666) na Morogoro (7,171), Dar es Salaam (1,717), Mbeya 1,549, Tabora 590 na Songwe 328.

Mikoa yenye matukio machache ni Kaskazini Pemba (5), Kusini Pemba (6) na Mtwara (22).

Dk. Bakari alisema TCRA imeendelea kubaini simu za ulaghai zinazoingia nchini na hatua stahiki zimekuwa zinachukuliwa ambapo idadi ya simu za udanganyifu imeendelea kupungua.

"TCRA imesimamia katika kuzuia matumizi ya simu zilizoripotiwa kuibiwa, kupotea au kuharibika pamoja na kuzuia matumizi ya simu zisizokuwa na viwango au za bandia.

"Usimamizi huu unawezesha kubaini na kufungia namba tambulishi za vifaa vya mawasiliano zilizonakiliwa (Duplicate IMEIs), namba tambulishi za vifaa vilivyotumika kwenye udanganyifu pamoja na namba tambulishi zilizotolewa taarifa ya kupotea au kuibwa," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema TCRA kupitia Kanzidata ya Namba Tambulishi (Central Equipment Identity Register- CEIR) zoezi hilo lilifanikiwa na kwamba TCRA imeendelea kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano ya simu na vyombo vya ulinzi na usalama, ili kubaini na kushughulikia uhalifu unaotendwa kupitia laini za simu.

Alisema mamlaka hiyo yenye dhamana ya kusimamia sekta ya mawasiliano nchini imeendelea kutoa elimu ya matumizi bora na salama ya simu kwa watumiaji wa huduma za mawasiliano ili kuwakinga dhidi ya matukio ya uhalifu mtandaoni.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, TCRA imeendelea kuwahimiza wananchi kuendelea kuripoti kwa njia ya ujumbe mfupi (SMS) simu zote zenye viashiria vya ulaghai au utapeli kwa kutuma namba husika "za matapeli" kwenda namba 15040 bila malipo.

# Waziri ashukuru Marekani kuirejesha Tanzania MCC

Na Benny Mwaipaja

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba ameshukuru Marekani kupitia Shirika lake la Changamoto za Milenia (MCC) kwa kuiteua Tanzania kuwa moja ya nchi zilizoko kwenye mpango wa kunufaika na ruzuku zinazolenga kusaidia mageuzi ya kisera na kitaasisi ili kutatua vikwazo vya ukuaji uchumi.

Dk. Nchemba alitoa shukrani hizo jana jijini Dar es Salaam alipokutana na kufanya mazungumzo na ujumbe wa MCC, ukiongozwa na Naibu Ofisa Mtendaji Mkuu wake, Chidi Blyeden.

Aliueleza ujumbe huo kuwa Tanzania imepiga hatua kubwa katika kusimamia uchumi wake, masuala ya utawala bora, haki za binadamu na demokrasia. Sasa imetekeleza kwa kiwango kikubwa vigezo vilivyowekwa na shirika hilo ili nchi iweze kunufaika na mpango huo.

Dk. Nchemba alishukuru MCC kwa mchango wake mkubwa katika maendeleo ya nchi ambapo kupitia Mradi wa Changamoto za Milenia uliotekelezwa nchini kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2008 hadi 2013, uliiwezesha Tanzania kupata Dola za Marekani milioni 698 zilizotumika kutekeleza miradi katika sekta za usafirishaji, nishati na maji.

"Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ameituliza nchi kisiasa na ana nia ya dhati ya kuituliza nchi kwa kuruhusu masuala ya kisiasa kufanyika kwa uwazi na hatua hii si tu kwa ajili ya kutekeleza vigezo vya taasisi yoyote, bali ni nia yake ya dhati ya kulinda uhuru wa watu," alisema.

Naye Naibu Ofisa Mtendaji Mkuu wa MCC, Blyeden, alipongeza Tanzania kwa hatua kubwa ilizopiga katika kuimarisha masuala ya utawala bora, demokrasia na haki za binadamu chini ya utawala wa Rais Samia, hatua iliyolifanya shirika lake kurejesha ushirikiano na serikali.

Alisema wataalamu kutoka MCC wanaendelea na mijadala na wataalamu wa serikali ili kuharakisha kuanza kwa utekelezaji mpango huo ambao matokeo yake hapo baadaye utaiwezesha Marekani kurejesha mradi wa Changamoto za Milenia (MCC-Compact) ambao utakuwa na lengo la kusaidia nchi kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ya maendeleo.

Desemba mwaka jana, Bodi ya MCC ilizichagua Tanzania na Ufilipino kama wabia wake katika kuandaa programu za awali zitakazolenga katika mageuzi ya kisera na kitaasisi ambazo nchi hizi zinaweza kuyafanya ili kupunguza umaskini na kuchochea ukuaji wa uchumi.

Bodi hiyo ya MCC ilichukua uamuzi huo baada ya Tanzania na Ufilipino kuonesha dhamira mpya ya kusukuma mbele mageuzi muhimu ya kuimarisha utawala wa kidemokrasia, kulinda haki za binadamu na kupambana na rushwa.

MCC ni shirika huru la Serikali ya Marekani linalojielekeza kupunguza umaskini duniani kupitia ukuaji wa kiuchumi kwa kutoa ruzuku na misaada ya muda maalum kwa nchi zinazokidhi viwango na vigezo thabiti vya utawala bora, mapambano dhidi ya rushwa na kuheshimu haki za kidemokrasia.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA

# Hatua zichukuliwe kukomesha michango holela shuleni

**MPANGO** wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano uliweka kiwango halisi cha uwiano wa uandikishaji elimu ya msingi kuwa asilimia 100 kufikia mwaka 2022.

Vilevile, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26), mbali na mambo mengine, umebainisha malengo muhimu katika sekta ya elimu yanayotakiwa kufikiwa ifikapo mwaka 2026.

Hayo ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari kama vile ujenzi wa vyumba vya madarasa, ununuzi wa madawati na vitabu, kuboresha uwiano wa vyoo na mazingira ya kazi kwa walimu katika ngazi zote, malipo yao na makazi kuwa karibu na maeneo ya kazi.

Kukiwa na mikakati hiyo ya kisera, jana tuliripoti kuhusu walimu 17 wa shule za msingi na sekondari jijini Mbeya ambao wamechukuliwa hatua za kinidhamu kwa kukiuka miongozo ya serikali, wakibainika kutoza michango ya madawati kwa wanafunzi ili wawaandikishe kuanza shule.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa ndiye aliyebainisha dosari hiyo ya kiutendaji wakati wa Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya. Kati ya walimu hao, wanane ni wa shule za msingi na tisa ni sekondari za jiji hilo.

Kimsingi, kilichobainika jijini Mbeya ndiyo uhalisia katika maeneo mengi nchini. Kumekuwa na kilio cha wazazi na walezi kutakiwa kutoa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shule ilhali Bunge limeshapitisha bajeti kwa ajili ya suala hilo.

Hivi karibuni, Nipashe tuliripoti kuhusu uongozi wa Shule ya Wasichana Shinyanga kutoza mchango wa Sh. 80,000 kwa kila mwanafunzi anayejiunga nao, tozo ikibatizwa jina la 'mchango kwa ajili ya uendeshaji wa shule.

Mwaka 2022 tuliripoti kadhia kama hiyo katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Ashira, mkoani Kilimanjaro ambako serikali pia ilichukua hatua ya kuzuia michango hiyo kama ilivyofanya kwa Shule ya Sekondari ya Wasichana Shinyanga mwaka huu.

Tukiwa wadau wakuu wa ustawi wa elimu nchini, tunaunga mkono hatua zilizochukuliwa na serikali kuzuia michango holela shuleni, ikizingatiwa tayari Bunge limeshaidhinisha bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Utoaji Elimumsingi Bila Malipo, maarufu elimu bure.

Tunatambua pia kwamba baadhi ya walimu na kamati/bodi za shule wanalazimika kuwa na michango hiyo katika shule zao kutokana na serikali ama kutotoa fedha za utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Malipo au kutoa fedha pungufu.

Hivyo, tunashauri hatua stahiki zichukuliwe kuhakikisha kunakuwa na uwajibikaji katika utoaji elimu nchini na kutokwaza utekelezaji wa mikakati ya serikali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Itungwe sheria kukomesha utoro

Na Sabato Kasika

**VIONGOZI** wa serikali kuanzia wakuu wa wilaya na mikoa wametangaza msako kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza ambao hawajaripoti shuleni tangu shule zifunguliwe Januari 8, mwaka huu.

Kwa sasa kila kona ni matangazo ya viongozi hao ya kuanzisha msako na kuchukulia hatua wazazi na walezi ambao watoto wao hawajaripoti shule, lengo ni kila mwanafunzi aliyechaguliwa kuanza kidato cha kwanza ahudhurie katika shule aliyopangiwa.

Matangazo hayo ya kufanya msako na kuwachukulia hatua wazazi na walezi ni ya kila mwaka kwa lengo la kutaka wanafunzi wa kidato cha kwanza wasiohudhuria masomo katika shule walizopangiwa kwa wakati.

Ninadhani kwamba, ipo haja ya kutafuta mbinu nyingine ambazo zinaweza kumaliza utoro huo ambao unaonekana kuota mizizi na kusababisha kiwango cha elimu kushuka kwa wanafunzi wenyewe.

Ninadhani ikiwezekana, wazazi na walezi waelimishwe kuhusu umuhimu wa elimu ili wawe wanawaandaa watoto wao mapema kwa ajili ya kuanza kidato cha kwanza.

Hatua hiyo itawafanya watimize wajibu wao kikamilifu badala ya kusubiri wasakwe au wasukumwe na viongozi wa wilaya au mkoa kupitia msako wa wanafunzi watoro.

> **Hatua hiyo itawafanya watimize wajibu wao kikamilifu badala ya kusubiri wasakwe au wasukumwe na viongozi wa wilaya au mkoa kupitia msako wa wanafunzi watoro.**

Ninaamini kwamba, wapo baadhi ya wazazi na walezi wasiojua umuhimu wa elimu, hivyo si vibaya wakaelimishwa badala ya kusakwa na kuwekwa ndani wakati hawajui lolote kuhusu elimu.

Wakati mwingine hao ndio ambao wanasomesha watoto wao elimu ya msingi, kisha wanawaacha badala ya kuwawezesha kuendelea na masomo ya sekondari na kujikuta wakiwa watoro na kuanza kusakwa.

Hivyo, ninadhani msako tu hautakuwa na matokeo chanya, badala yake elimu itolewe viongozi wa ngazi ya chini katika vijiji wahusike, kwa sawa wanawajua wa maeneo yao, lakini wazazi na walezi waelimishe wajue faida ya elimu kwa watoto wao.

Katika wilaya ya Nachingwea, mkuu wa wilaya hiyo, Mohamed Hassan Moyo ameshatangaza kuwachukulia hatua wazazi na walezi ambao watoto wao bado hawajaripoti kidato cha kwanza.

Vilevile, si viongozi kuanzia ngazi ya vitongoji wakawa wanahusika kujua idadi ya wanafunzi waliochaguliwa kwenda sekondari katika maeneo yao ili wasaidie kutia msukumo. Jukumu la viongozi hao linaweza kuwa la kuwahimiza wazazi na walezi kuwaandaa watoto wao na kuwambusha umuhimu wa shule ili zinapofunguliwa, wote waanze masomo kwa wakati.

Kupitia njia hiyo ya kutoa elimu na kushirikisha viongozi wa ngazi ya chini, ninadhani kunaweza kuwa na matokeo chanya katika kukomesha utoro katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Inasikitisha kusikia wanafunzi wanachaguliwa kuanza kidato cha kwanza halafu hawaendi shule. Wanakuwa wapi? Wazazi na walezi wangeelimishwa wajiue wajibu wao kwa watoto kuhusu elimu.

Ni vyema kujua kundi hilo kubwa la wasioanza kidato cha kwanza linakwenda wapi wakati huu ambao serikali inatoa elimu bure ikiwa ni fursa ya kutaka wanafunzi wote wa Kitanzania wanaipata.

Kwa njia hiyo, kama kuna familia zenye changamoto zinazoshindwa kupeleka watoto kupata elimu ya sekondari, kwa ukosefu wa fedha za kununua sare na vifaa vingine ya shule, zisaidiwe. Hivyo, msako wa wanafunzi watoro na kutunga sheria ya kuwashtaki wazazi, walezi na wote wanaokwamisha wanafunzi wasiende shule ni hatua za kufikiria.

Pamoja na kutangazwa, njia ya kuewalimisha na kuwahamasisha pia kuhusisha viongozi wa ngazi ya chini kusaidie kudhibiti utoro huo.

Ninaamini pengine hakuna mzazi au mlezi anayependa mtoto wake awe mtoro au asisome, labda wakati mwingine ni kutokana na kutoelewa umuhimu wa elimu au changamoto nyingine za maisha anazopitia.

HABARI KITAIFA

## Wenye kifafa walia na imani potofu katika jamii

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha Wataalamu wa Kifafa Tanzania (TEA) kimetoa rai kwa jamii kuondokana na imani potofu kuhusu ugonjwa huo, ikiwamo kuwatenga na kusababisha kukosa msaada kunakohatarisha uhai wao.

Bingwa wa Ubongo, Uti wa Mgongo na Mishipa ya Fahamu, Dk. Patience Njenje kutoka PCMC Kliniki aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam aliposoma tamko kwa niaba ya TEA.

Alisema wanaougua kifafa nchini wako katika hatari ya kifo mara sita zaidi kulinganishwa na jamii yote kwa ujumla, huku zaidi ya asilimia 60 ya vifo vikisababishwa na athari za ugonjwa moja kwa moja au namna nyingine.

"Watu wanaoishi na kifafa ni zaidi ya watu milioni 60 duniani kote na ni ongezeko la watu 34 hadi 76 kwa kila watu 100,000 kwa mwaka. Kaulimbiu ya 2024 ni 'Tulikotoka, tulipo na tunakoelekea'.

"Afrika ni mojawapo, ina asilimia kubwa ya watu wanaoishi na kifafa. Inafahamika ni watu 20-58 kwa kila watu 1,000. Tanzania ina idadi kubwa ya wagonjwa wa kifafa katika Afrika na dunia, ni moja kati ya nchi zenye wagonjwa wengi zaidi," alisema.

Bingwa huyo aliongeza kwamba kwenye vijiji vya Wilaya ya Mahenge, idadi ni kubwa hadi 37/1,000 na kufanya watu zaidi ya milioni moja Tanzania ambao wana ugonjwa wa kifafa.

Dk. Njenje alifafanua kwamba wagonjwa wengi wa kifafa ni vijana wakiwa na katika umri wa wastani wa miaka 15.

"Zaidi ya asilimia 25 ya wagonjwa wa kifafa wana ulemavu, hii husababishwa na kuanguka wakati wa ugonjwa anapopata degedege. Pamoja na ugonjwa kuwapo karne nyingi, idadi kubwa ya watu nchini wana imani potofu kuhusu kifafa.

"Na zaidi ya asilimia 36 bado wanaamini kwamba, ugonjwa wa kifafa unatokana na nguvu za giza. Asilimia 50 katika jamii wanaamini ni ugonjwa unaoambukiza."

Bingwa huyo alieleza pia kuwa watoto wenye umri wa kwenda shuleni wenye tatizo hilo kwa asilimia 45 hawapelekwi shuleni na asilimia 68 ya mahudhurio yao hayaridhishi huku asilimia 37 ndio hupata elimu ya msingi.

"Watoto hawa hawaruhusiwi kucheza na wengine, hivyo hufichwa katika jamii. Asilimia 75 ya wagonjwa huenda kuwaona waganga wa jadi na wengine huenda kuwaona viongozi wa kiroho (dini).

"Baada ya mgonjwa kuathirika kwa asilimia tano hadi 10 ndipo huweza kupata matibabu hospitalini na chanzo cha ugonjwa huu ni; homa kipindi cha utotoni, kwa watu wazima mara nyingi husababishwa na minyoo, uvimbe kwenye ubongo na baadhi ajali kichwani au upungufu wa kinga."

Alitoa angalizo kwamba si kila kuanguka ama kupoteza faharnu ni kifafa, huku akitoa mbinu za kujikinga na visababishi vinavyozuilika ni kama vile kumjali mama mjamzito kipindi chote cha ujauzito na kuhudhuria kliniki.

"Ugunduzi na matibabu ya haraka kwa watoto wanapopata homa, kuhimiza choo bora na kwa wale wanaokula nyama ya nguruwe iive, kuacha kuwabagua wagonjwa. Serikali ihakikishe kuwapo utoaji dawa za kutosha kutibu wagonjwa hawa.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (katikati), akikabidhi tuzo ya kuunga mkono jitihada za kufanikisha mradi wa kulinda vyanzo vya maji wa Ziwa Viktoria kwa Ofisa Mawasiliano wa Barrick, Neema Ndossi (wa pili kulia) na Ofisa Rasilimali wa North Mara, Eric Wambura (kulia) kwa niaba ya Mgodi wa Barrick North Mara, ambao umetunukiwa tuzo hiyo wakati wa ufunguzi wa mkutano wa wadau wa maji unaoendelea jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Waziri wa Maji, Jumaa Aweso. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil. 1/- zatumika kuboresha miundombinu iliyoharibiwa

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha Msalaba Mwekundu Tanzania kimetumia zaidi ya Sh. bilioni moja kuboresha miundombinu mbalimbali ilioharibiwa na mvua katika mikoa minne ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Manyara, Geita na Mjini Magharibi ambako chama hicho pia kimetoa huduma za kibinadamu kwa waathirika wa mafuriko hayo.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, Meneja wa Kukabiliana na Maafa wa chama hicho, Samwel Katamba alibainisha kuwa kati ya Sh. bilioni moja iliyotumika, Sh. milioni 269.21 zilitumika katika usafi wa maji na mazingira.

"Bajeti ya ujenzi wa nyumba na ujenzi wa vyoo na visima vya maji ilikuwa Sh. 709,377,000 wakati Sh. 93, 022,000 zilitumika kutoa huduma za afya na elimu ya kujikinga na magonjwa," alisema Katamba.

Alisema kaya 795 katika mikoa hiyo minne zimesaidiwa vitu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magodoro, mablanketi, vifaa vya jikoni, taulo za kike, vyandarua, dawa za kutibu maji na chakula.

"Wafanyakazi wa kujitolea bado wako katika mikoa hiyo wakiendelea kutoa elimu ya afya, elimu ya usafi wa maji na mazingira, matumizi mazuri ya maji na huduma ya saikolojia," alisema.

Meneja huyo alisema chama hicho kinatarajia kutoa Sh. milioni 108 kwa machinga 180 wa Mkoa wa Manyara ambao biashara zao ziliharibiwa na mafuriko ya mvua hiyo.

Meneja huyo alifafanua jinsi msaada huo utakavyotolewa kuwa kila mfanyabiashara mdogo atakuwa anapewa Sh. 100,000 kila mwezi kwa muda wa miezi sita ili waweze kuboresha biashara zao.

Katamba aliongeza kusema kuwa kwa hesabu hiyo, katika kipindi cha miezi sita chama chao kitakuwa kimetumia Sh. milioni 108, kwa ajili ya wafanyabiashara hao

"Kwa sasa kinachoendelea sasa ni kuwaingiza katika mfumo tunaotumia, unaitwa KOBO ambao pia unatumika kimataifa, na tunatarajia kuanza kuwapa kuanzia mwishoni mwa mwezi huu," alisema.

## Miti 20,000 kupandwa kukabili athari za mabadiliko ya tabianchi

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

CHUO Kikuu Mzumbe mkoani Morogoro kimeanza kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kupanda miti, kikipanga kuanza na upandaji miti 20,000 katika maeneo yanayozunguka chuo hicho ili kuhifadhi mazingira na kurudisha uoto wa asili.

Katika uzinduzi wa kampeni ya upandaji miti 3,000 uliofanyika Kampasi Kuu ya chuo hicho iliyoko katika Kijiji cha Changarawe, Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. William Mwegoha, alisema lengo la kampeni hiyo ni kulifanya eneo hilo kuwa la kijani.

Prof. Mwegoha alisema kuwa kwa kuanzia, miti 20,000 itapandwa kwenye Kampasi Kuu ya Morogoro na baadaye itapandwa kwenye kampasi zingine za Mbeya na Dar es Salaam ili kusaidia kumaliza changamoto ya uharibifu wa mazingira na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Sisi familia ya wana Mzumbe leo (jana) tumeanza rasmi kampeni yetu ya kupanda miti 20,000. Kwa kuanzia, tunaanza kupanda miti 3000, na zoezi hili litaendelea hadi kufikia malengo yetu ya kuifanya Mzumbe kuwa ya kijani," alisema Prof. Mwegoha.

Makamu Mkuu wa Chuo alisema Rais Samia alipokuwa Zanzibar hivi karibuni, alitoa maelekezo ya kupanda miti kila mwezi, hivyo wametekeleza agizo hilo.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Changarawe, Fredinand Matangalu, alisema watashirikiana na Mzumbe kuhakikisha mifugo na watu wanaofanya kilimo hawafanyi uharibifu wowote ili miti hiyo istawi.

"Sisi kama Serikali ya Kijiji hiki cha Changarawe ambacho Chuo Kikuu Mzumbe kimo, tutahakikisha hii miti inakua kwa malengo yaliyokusudiwa. Chuo hiki kimekuwa kinatushirikisha kwa mambo mbalimbali ya kimaendeleo," alisema.

Naye mwanafunzi wa mwaka wa pili anayechukua shahada ya mazingira, Halima Mzinga, alisema kampeni hiyo ya kupanda miti inapaswa kuwa endelevu ili kurudisha uoto wa asili na kupambana na uharibifu wa mazingira katika Mkoa wa Morogoro.

Alishauri Jamii kuzingatia umuhimu wa kupanda miti na kuitunza katika maeneo mbalimbali ya mkoa ili kusaidia upatikanaji mvua ambao utasaidia kwenye shughuli za kilimo na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo hicho cha Mzumbe - Mipango, Fedha na Utawala, Prof. Allen Mushi, alisema wameweka mikakati ya kuhakikisha miti hiyo inalindwa ili isichomwe moto au kuharibiwa kutokana na shughuli za kibinadamu.



Wananchi wa Kata ya Songe, Wilaya ya Kilindi, Mkoa wa Tanga wakifyeka mahindi kwenye eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari Seuta kidato cha tano na sita katika Kijiji cha Songe, serikali imetoa zaidi ya Sh. milioni 400. **PICHA: DEGE MASOLI**

# Mnyeti asema kuna wakurugenzi wavivu kuomba fedha za miradi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa baadhi ya wakurugenzi wa halmashauri ni wavivu kuwasilisha maombi ya fedha za ujenzi wa majosho kwenye maeneo yao kwa Wizara ya Fedha licha ya kujulishwa kuwapo fedha hizo.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti, alitoa kauli hiyo bungeni wakati akijibu maswali ya Mbunge wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu yaliyoulizwa kwa niaba na Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Aysharose Matembe.

Mbunge huyo alisema serikali mwaka huu wa fedha imeahidi kujenga majosho katika vijiji vya Siuyu, Ulyampiti, Isuna na Visule, lakini hadi sasa hayajajengwa na hata zabuni haijatangazwa, akihoji lini mchakato huo utafanyika.

Pia alihoji lini serikali itajenga majosho kwenye vijiji vya Jimbo la Singida Mashariki ili kulinda afya za mifugo.

Akijibu maswali hayo, Mnyeti alisema wizara imeshatoa maelekezo kwa wakurugenzi wote nchini ambao walitengewa bajeti ya ujenzi wa majosho, fedha zipo, wanachotakiwa ni kupeleka maombi ili wapatiwe.

"Ninawaomba wabunge wanapokuwa kwenye vikao vya kamati za fedha na mipango kwenye halmashauri, wawe wakali kuwasukuma wakurugenzi kuomba hizi fedha.

"Baadhi ya wakurugenzi ni wavivu, wanashindwa kuziomba hizi fedha, zipo tayari, wengine tayari lakini wengine wavivu ndio bado, hali inayosababisha kuwa na mrundikano mwingi wa fedha kwenye halmashauri," alisema.

Naibu Waziri alisema wizara imeshaanza kutoa elimu kuhusu ufugaji bora wa kisasa na kuachana ufugaji wa zamani wa kufuga ng'ombe wengi wasio na tija na hilo limeshafanyika mikoa mbalimbali.

Alisema serikali inaendelea na mpango wa ujenzi wa majosho nchini ili kudhibiti magonjwa yanayoenezwa na kupe na wadudu wengine na katika mwaka wa fedha 2023/24, wizara ilitenga Sh. bilioni 5.7 kwa ajili ya ujenzi wa majosho 246 katika halmashauri 63 nchini.

"Katika Jimbo la Singida Mashariki mwaka 2022/23, serikali ilijenga majosho manne ambayo ujenzi wake ulikamilika na yanafanya kazi na mwaka 2023/24, majosho manne yanajengwa katika vijiji vya Ndughamunga, Unyampanda, Ughandi na Ngamu vilivyoko Kata za Mughunga, Ughandi na Mwasauya," alisema.

# Gavana BoT apongeza kanuni mpya za usimamizi wa fedha

**Na Joseph Mwendapole**

UMOJA wa Benki Tanzania (TBA) umefanya kongamano la pili la ujumuishi wa kifedha ambalo limewaleta wadau katika sekta ya fedha pamoja kujadili fursa, changamoto na namna ya kuwafanya Watanzania wengi watumie huduma za kifedha hususani za kibenki.

TBA pia imezindua Kanuni za Usimamizi Endelevu wa Sekta ya Fedha, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Emmanuel Tutuba, akipongeza benki kwa kuja na kanuni ambazo pamoja na mambo mengine zitakuwa na mchango mkubwa katika kuongeza ujumuifu kwenye sekta ya fedha.

Gavana Tutuba aliyekuwa mgeni rasmi katika kongamano hilo, alisema kanuni hizo zitaongeza ujumuishi hasa kwa makundi ambayo yamekuwa yakiachwa nyuma na hivyo kuongeza idadi ya Watanzania ambao wako kwenye mfumo rasmi wa kifedha.

"Tangu tumezindua Mpango wa Tatu Jumuishi wa Sekta ya Fedha, tumefikia asilimia 76, lakini lengo letu ni kufikia asilimia 85 kufikia mwaka 2028. "Kanuni hizi zitasaidia benki na taasisi za kifedha kutelekeza majukumu yao na kuyagusa makundi ambayo yameachwa nyuma," alisema.

Gavana alizihakikishia benki ushirikiano kuwa BoT itaendelea kuwa mstari wa mbele kufanya kazi nayo na kutengeneza mazingira rafiki kwa benki kufanya shughuli zake. Mwenyekiti wa TBA, Theobald Sabi alisema benki zinafahamu kuwapo makundi hayo ikiwa ni pamoja na wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambao wameachwa nyuma kwenye huduma za kifedha na kusema mkutano huo utajadili namna bora ya kuyajumisha.

"Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia tunaamini kuwa sisi sekta ya benki tunaweza kuyafikia makundi maalum ambayo hayajafikiwa na kwa gharama nafuu," alisema.

Katika kongamano hilo, Gavana wa BoT pia alizindua Kanuni za Utumiaji Fedha Endelevu (Sustainable Finance Principles (SFPs) zilizotengenezwa na TBA kwa kushirikiana na washirika wa BOT.

# Sheria ya Ushindani kufumuliwa kimkakati

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo, Mifugo na Uvuvi imebariki mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Ushindani ambayo pamoja na mambo mengine yanalenga kutoa rukhsa ya muungano wa kampuni usiodhoofisha ushindani.

Vilevile, kamati hiyo imeitaka Tume ya Ushindani (FCC) kuendelea kuweka nguvu ya kudhibiti bidhaa bandia nchini kwa kuwa zinaikosesha serikali mapato.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Deo Mwanyika aliyasema hayo juzi baada ya kamati kupokea wasilisho la utendaji kazi wa FCC jijini hapa.

"Tunakubaliana kwamba sheria ile iliyounda tume hii ifanyiwe maboresho kutokana na maeneo mengi teknolojia imebadilika na idadi ya wawekezaji wa ndani na nje imeongezeka tangu Rais Samia aingia madarakani," alisema.

Mwanyika alisema mambo yaliyowasilishwa na tume hiyo kwenye kamati kuhusu maboresho ya sheria hiyo yanakwenda kuongeza tija na kuhakikisha biashara inafanyika kwa usawa.

Alisema kamati inapongeza hatua zinazochukuliwa na tume hiyo katika kudhibiti bidhaa bandia kwa kushirikiana na taasisi zingine na kuwaomba Watanzania kutoa ushirikiano ili kuondoa bidhaa hizo.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaudi Kigahe, alisema tume hiyo inapanga kusaidia kudhibiti biashara ya bidhaa feki kwa kuwa bado kuna changamoto kubwa inahitajika kufanya kazi ya ziada.

Awali Mkurugenzi Mkuu wa FCC, William Erio, alisema moja ya majukumu ya tume ni kumlinda mlaji dhidi ya kudhibiti bidhaa bandia.

"Tumeiambia kamati maeneo yenye mrengo wa kisheria yanayopaswa kuboreshwa ili kuongeza ufanisi kwenye utendaji kazi, tumewasilisha serikalini na mchakato umepita ngazi zote za serikali, sasa unakwenda ngazi ya Bunge ili kubadilisha Sheria ya Ushindani ambayo ilitungwa mwaka 2003," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema sheria hiyo kwa sasa ina miaka 21 na mazingira ya uwekezaji kwa kipindi cha nyuma yalikuwa tofauti na ilivyo sasa ikizingatiwa kuwapo Sera mpya ya Uwekezaji.

"Tutabadilisha na kuweka eneo jipya la muungano wa kampuni kwamba muungano huo usidhoofishe ushindani, tumeangalia asilimia ya kuongezeka kwa soko kutoka asilimia 35 ikiwezekana iende hadi asilimia 40 kama itaridhiwa na Bunge," alisema. Kuhusu bidhaa bandia, alisema tume imepewa jukumu la kudhibiti uingizwaji bidhaa bandia, kuzuia uzalishaji wake, kusambazwa au kupitishwa nchini kwenda nchi jirani.

"Tunashirikiana na BRELA zile bidhaa zilizosajiliwa mtu asiende kutengeneza zikaonekana kama bidhaa halisi kumbe si halisi, tumeanza kutoa elimu watu waelewe madhara ya bidhaa bandia kwa kuwa zinaikosesha serikali kodi, zinafanya wafanyabiashara halali kufunga biashara zao kwa kushindwa kushindana na bidhaa bandia," alisema.





## Mkenda ahimiza uwekezaji kwenye masomo ya sayansi

**Na Getrude Mpezya,** ARUSHA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, ameitaka jamii kuwekeza zaidi kwenye masomo ya sayansi, ambayo yatawapatia vijana fursa za ajira na kukua kiuchumi.

Wito huo aliutoa jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake na Wasichana katika sekta ya sayansi mkoani Arusha kwa kauli mbiu ya "Wanawake na wasichana katika uongozi wa sayansi enzi mpya ya maendeleo endelevu."

Prof. Mkenda alisema ili kuendana na kasi ya teknolojia wazazi na walezi wanapaswa kujikite kuwawekea mazingira rafiki watoto wa kike kwa kuwa itawajenga kupenda masomo hayo.

Prof. Mkenda alisema kuwa wanawake na wasichana ni watu muhimu kwa mustakabali wa sayansi iliyobora kwa kuwa hupelekea upatikanaji wa ajira ya uhakika kutokana na kubuni vitu mbalimbali vitakavyosaidia nchi kwenye ubunifu.

"Tunapoteza sana kama nchi kwa kutokuwapa nafasi wasichana wengine kwenda kusoma masomo ya sayansi kwa kuwa unaweza kuwa mjasiriamali, lakini bila sayansi na teknolojia hatuwezi kufika mbali tunatakiwa kuwekeza kwa elimu ya sayansi kwa sababu wenzetu wamejiwekeza katika elimu hiyo," alisema.

Hata hivyo, alisema fursa za kazi duniani huko tuendako zitategemea elimu ya TEHAMA hivyo wasipofundisha vijana katika eneo hilo, kutawanyima nafasi za kupata ajira.

"Wizara ya elimu imejipanga vizuri kuendelea kutekeleza ufadhili kwa wahitaji wote kwa kuwa sisi na wadau wa elimu tutakuza sayansi hapa nchini na tutafanya kila liwezekanalo wasichana wengi kusoma masomo ya sayansi ili kukuza uchumi wetu.

"Tunatoa tuzo ya fedha kwa watafiti katika maeneo ya sayansi (utafiti), ukifanya kazi yako ukaweka sehemu kubwa zinazofahamika unapewa Sh.milioni 50, pia ninapenda kuona watu wanasoma sayansi zaidi, kwa kuwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amewekeza kwenye ujenzi wa shule za sayansi na mabweni ili wapate elimu nzuri," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wadau wa elimu, Prof. Juma Hatibu, kutoka Shule ya Sekondari ya Sayansi ya Arusha, alisema suala la ubunifu ni jambo muhimu kwa kuwa inasaidia kuleta ajira kwa vijana wa Kitanzania na kufungua fursa kwenye miradi mbalimbali.

Mwakilishi wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Jovian Mley, alisema maendeleo endelevu ya eneo nyeti la sayansi wananchi wanapaswa kujua kufanya mjadala wa masomo ya sayansi kwa watoto wa kike kwa kushirikishwa shughuli zote katika vyuo, shule za msingi na sekondari.

Profesa Mstaafu wa Somo la Hisabati wa Chuo cha Nelson Mandela na Mwenyekiti wa Bodi ya Misitu Tanzania,Verdiana Masanja, alisema kwa miaka mingi wasichana walikuwa nyuma lakini kumekuwa na mabadiliko makubwa kati ya elimu ya mwanamke na mvulana jambo ambalo linawasaidia wao kama wadau wa elimu kuona tofauti kati ya miaka ya sasa na zamani.

Mshiriki na Mwanafunzi wa Shule ya Sayansi ya Arusha, Rose Mziray, alisema baadhi ya changamoto inayochangia kutokutambulika kwa elimu sayansi ni pamoja na mila na destuli ambazo zinawakandamiza wasichana kutokufikia malengo kielimu.

# Mpango awataka viongozi wa dini kuongeza bidii kuelekeza waumini

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amewaomba viongozi wa kanisa kuongeza bidii ya kuchunga kundi la waumini wanaowaongoza kwa kuwa viongozi hao watatoa hesabu ya kazi waliyofanya siku moja mbele ya Mungu.

Aliyasema hayo juzi jijini Arusha, wakati akitoa salamu za serikali katika ibada ya kumwingiza kazini Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini Kati, Dk.Godson Abel, iliyofanyika katika Usharika wa Kimandolu mkoani humo.

"Neno la Mungu linawataka viongozi wa kanisa kufanya bidii katika kuifanya kazi ya Mungu hasa kulitumikia kundi walilokabidhiwa na mkikumbuka kuwa siku moja mtaitolea hesabu kazi yenu mliyoifanya mbele za Mungu," alisema Dk. Mpango. Hata hivyo, aliitaka Wizara ya Afya, kutatua matatizo yanayokwamisha ubia kati ya serikali na Hospitali ya Lutherani ya Seliani iliyoko jijini Arusha (ALMC), kwa lengo la kuleta ufanisi wa huduma katika hospitali hiyo ambayo inamilikiwa na Dayosisi ya Kaskazini Kati.

Pia alimkabidhi askofu mpya zawadi ya pongezi ya Sh. milioni 10 kwa hatua ya kuingizwa kazini kwa ajili ya kuwatumikia waumini wa kanisa hilo.

Licha ya kuzungumza hayo, alimwagiza Meneja wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Arusha, kuanza mara moja kuweka lami kipande kidogo cha barabara ya kuingia katika kanisa hilo.

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Alex Malasusa, alisema huduma za afya zinazomilikiwa na kanisa hilo ni nyingi katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Alisema ni matumaini yao kwamba endapo serikali itatatua matatizo yaliyopo ikiwamo mkwamo ya ushirikiano kati ya serikali na vituo kwa kuwa itasaidia huduma kuwa bora zaidi.

Awali akihubiri katika ibada hiyo, Askofu wa Anglikani Dayosisi ya Mount Kilimanjaro, Stanley Hotay, aliiomba serikali kufungia baadhi ya mitandao ya kijamii inayopotosha maadili ya Kitanzania hasa kwa suala kwa suala la ushoga.

"Niombe viongozi wa serikali kuifungia baadhi ya mitandao ambayo imekuwa ikipotosha maadili kwa kuwa unakuta watoto wetu, wanapotea kwa kuangalia mitandao hii ambayo muda mwingi inaangazia habari za ushoga na maadili mengine ambayo hayafai katika nchi yetu," alisema. Licha ya kuzungumza hayo, aliitaka jamii kuwakumbuka na kuwasemea watoto wakiume kwa kuwa wanaopewa kipaumbele ni watoto wakike huku akisema kuwa watoto wakiume wamesahaulika na hawana wakuwasemea.



Ofisa wa Polisi Kata ya Songe, Wilaya ya Kilindi, Mkoa wa Tanga, Msaji Mwaswengu, akijibu hoja mbalimbali kutoka kwa wananchi wa kata hiyo mwishoni mwa wiki kwenye mkutano wa hadhara wa Kijiji cha Songe. **PICHA: DEGE MASOLI**

# Udumavu Arusha waishtua serikali

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Arusha, Missaile Mussa, amewataka wajumbe wa kamati ya lishe mkoani humo, kuongeza wigo wa kutoa elimu kwenye jamii ili kupunguza idadi ya watoto wenye udumavu kwa kuwa changamoto hiyo inayojitokeza zaidi maeneo ya vijijini katika mkoa huo.

Aliyasema hayo wakati akifungua kikao cha lishe mkoa wa Arusha kwa ajili ya kuwasilisha taarifa za afua za lishe kwa kipindi cha robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mussa alisema licha ya kuwapo kwa changamoto ya udumavu kwa watoto, lakini kuna mabadiliko kiasi ingawa watoto wa maeneo ya vijijini wanakabiliwa na hali ngumu zaidi kutokana na uhaba wa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa lishe kwa watoto walio chini ya umri wa miaka miwili na miezi saba.

Kutokana na hali hiyo aliwataka wataalam kwa kushirikiana na wadau wa elimu kupanua wigo kwa kuwafikia wananchi wengi zaidi kuwaelimisha umuhimu wa lishe.

"Bado mkoa wetu unakabiliwa na changamoto ya utekelezaji wa afua za lishe kutokana na sababu mbalimbali, hivyo niwatake wataalamu kuongeza wigo katika utoaji wa elimu kwa jamii na tufanye kazi kwa bidii ili kukabiliana na changamoto hii ya udumavu kwa watoto," alisema Katibu Tawala huyo.


Hata hivyo, alizitaka halmashauri zote za mkoa huo kuipa kipaumbele ajenda ya lishe, ikiwa ni pamoja na kupeleka fedha za kutekeleza afua za lishe kwa asilimia 100 kwenye maeneo yao kwa wakati kama inavyoelekezwa kwenye bajeti zao.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa afua za lishe kwa kipindi cha mwaka 2023/2024, Mratibu wa Lishe Mkoa wa Arusha, Doto Milembe, aliahidi kuendelea kupambana na udumavu kwa mpango mikakati wa kuendelea kutoa elimu hasa kwa wajawazito kupitia vikao mbalimbali, kliniki pamoja na mikutano inayoendeshwa kwenye ngazi ya jamii.

"Tunaendelea kuhamasisha kinamama na jamii kwa ujumla juu ya umuhimu wa ulaji wa makundi sita ya vyakula, ili kupata virutubisho vinavyopaswa kwa watoto pamoja na kuongeza idadi ya milo kwa watoto hadi kufikia milo mitano inayoshauriwa kitaalamu," alisema mratibu huyo.

Aidha, wadau walioshiriki kikao hicho, walishukuru serikali kwa kuwa na mwamko wa kuhimiza umuhimu wa lishe kwa jamii na ushirikishwaji wa wadau jambo ambalo linarahisisha kuifikia jamii kwa pamoja kuliko kufanya kazi wenyewe.

Sheikh wa Wilaya ya Arusha, Hussein Said Ijunje, ambaye alimwakilisha Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Arusha, licha ya kuwapongeza wataalamu kwa kazi wanayoifanya alishauri kuongezwa nguvu zaidi ili kuwafikia wananchi wengi zaidi kwenye kata, vijiji na vitongoji na kushirikisha viongozi wa dini kwa kuwa wana ushawishi mkubwa kwenye jamii.



# Wahudumu Afya wadaiwa kunyanyapaa makundi maalum

**Na Timothy Itembe,** MARA

BAADHI ya wahudumu wa afya wilayani Tarime mkoani Mara, wamedaiwa kutofuata taratibu na weledi kwenye kazi kwa kuwanyanyapaa makundi maalum yanayotakiwa kupata huduma za matibabu bure.

Kauli hiyo imetolewa juzi na Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini, Mwita Waitara baada ya kumalizika kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Tarime.

Alisema ni muhimu wahudumu wakaacha tabia ya unyanyapaa hiyo mara moja na kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria.

Alisema sera ya afya inasema huduma za matibabu ni bure kwa wazee wenye umri wa miaka 65 kuendelea, watoto chini ya miaka mitano na wanawake wajawazito, lakini kwenye utekelezaji ni tofauti kwa kuwa wanatakiwa kupata fedha ndio wahudumiwe.

Alidai cha ajabu ni kuwa endapo wakihudumiwa bure basi wanaambiwa kanunue dawa kwenye vibanda vya watu binafsi pembeni mwa vituo husika wakidai vituo hivyo havina dawa ilihali serikali imesambaza dawa na vifaa tiba katika maeneo yote.

Alitoa mfano wa mgonjwa mmoja aliyepatiwa huduma katika eneo la Sirari kwa kufanyiwa upasuaji wa mguu, lakini alidaiwa hela kubwa ambayo haikuwa kwenye utaratibu hivyo kumfanya mgonjwa huyo ahangaike kupata. Aidha, aliwataka wale wote ambao wanatendewa vitendo kama hivyo watoe taarifa kwenye mamlaka husika, ili watoa huduma kama hao wachukuliwe hatua za kisheria mapema kabla tabia zao hazijaota mizizi.

Katika kikao hicho, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Tarime Vijijini, Samweli Kiles, aliwataka madiwani pamoja na watumishi kuendelea kutoa ushirikiano ili bajeti iliyokasimiwa ikipitishwa na bunge itekeleze miradi kwa wakati na kwa ufanisi.

Awali, akiwasilisha mapendekezo ya bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 Ofisa Mipango, Modest Lema, alisema kuwa bajeti imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele na miongozo yote ya bajeti na itaenda kujumuisha pia gharama za miradi viporo.

"Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 halmashauri inaomba kuidhinishiwa kukusanya na kutumia zaidi ya Sh. bilioni 49.1 ambapo vyanzo vya ndani ni zaidi ya Sh. bilioni 7.5, mapato lindwa zaidi ya Sh. bilioni 2.79 na jumla ya mapato ya dani ni Sh. bilioni 10.34,"alisema Lema.

Lema alitaja matumizi mengineyo kuwa Sh. bilioni 1.4, mishahara Sh. bilioni 25.3, jumla ya mapato ya ruzuku Sh. bilioni 38 na jumla kuu Sh. bilioni 49.1.



Mbunge wa Jimbo la Manonga, wilayani Igunga, mkoani Tabora, Seif Gulamali, akizungumza na wananchi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika viwanja vya Kata ya Choma mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMBE ISMAILLY**

# Wanafunzi wa kike waomba Shy kujengwa bweni kutokomeza zero

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANAFUNZI wa kike 375 wa Shule ya Sekondari Ingwamanoni Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wameiomba serikali kukamilisha ujenzi wa mbweni lililoanzishwa kwa nguvu za wananchi, ili kuondokana na kutembea umbali mrefu kufuata shule hiyo.

Wametaja safari hiyo ya muda mrefu imekuwa ikiwasababisha matatizo mbalimbali zikiwamo mimba na ndoa za utotoni hivyo ujenzi wa bweni utawasaidia kutimiza malengo yao.

Walitoa ombi hilo juzi kwa nyakati tofauti na kuitaja shule hiyo kuwa na ufaulu hafifu upande wa wasichana kila muhula kulinganisha na jinsia kiume na kudai kuwa kupatikana kwa bweni kutatatua tatizo hilo.

"Kutoka Kijiji cha Kipangu tunalazimika kutembea zaidi ya umbali wa kilometa 10 kwend a na kurudi shuleni hali inayotufanya tunachoshwa na safari na kushindwa kujisomea tunapotoka shule," alisema Sauda Ramadhani.

Alisema wanafunzi ambao wazazi wao wanauwezo wamewapangishia vyumba katika vijiji vilivyopo jirani na shule na kutaja hali pia kuwa hatarishi katika safari ya masomo yao kutokana na vishawishi wanavyokabiliana navyo. Joyce William alitaja hali ya mvua kuwa pia kero inayowasibu na wakati mwingine kushindwa kufika shule kabisa kutokana na ubovu wa barabara zinazojaa maji pamoja na mvua zinazonyesha bila kukatika.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Paul Ndalo alikiri kuwepo kwa adha hiyo na kutaja wanafunzi wa kike kuongoza kwa utoro na kufanya vibaya kwenye masomo yao. Kufuatia hali hiyo Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, aliendesha harambee iliyosaidia kupatikana kwa Sh. milioni 20 na kuwapongeza wazazi na walezi kwa kuona adha hiyo na kuanzisha ujenzi huo kuwanusuru watoto wa kike.

Alitoa ombi kwa wananchi baada ya kukamilika kwake basi waanzishe ujenzi wa bweni lingine m kwa ajili ya wanafunzi wa kiume pia.

# Watoto kupatiwa chanjo ya surua, rubella Tabora

**Na Halima Ikunji,** TABORA

WATOTO 544,616 wenye umri chini ya miaka mitano mkoani Tabora wanatarajia kupatiwa chanjo ya surua na rubella kuanzia Februari 15 hadi 18, mwaka huu, lengo likiwa ni kupunguza au kutokomeza kabisa vifo vya watoto.

Akizungumza katika kikao cha Kamati ya Afya ya Msingi Mkuu wa Wilaya ya Igunga, Sauda Mtondoo, alitoa jukumu kwa viongozi mbalimbali kuhamasisha wananchi kuhusu kampeni hiyo ya kitaifa.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Afya inaratibu chanjo hiyo, ikiwa ni mkakati wa kutokomeza maradhi na kupunguza vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano, hivyo kupunguza gharama kubwa zinazotumika katika matibabu.

Mtondoo alisema utafiti uliofanywa umethibitisha kuwa chanjo huzuia takribani vifo milioni 3 vitokanavyo na maradhi yanayokingwa kwa kila mwaka duniani.

Alitaja pia kwa Tanzania kuwa mafanikio ya chanjo yameonekana na kutokomeza ugonjwa wa ndui, dondakoo, kifaduro na pepo punda ambayo yamepotea kabisa kutokana na chanjo zilizotolewa zaidi ya asilimia 90 ya watoto nchini.

Kadhalika, alibainisha kuwepo kwa tatizo la baadhi ya wazazi kutokuwapeleka watoto kupata chanjo huku wengine wakishindwa kukamilisha ratiba ya chanjo kulingana na umri wa watoto wao hivyo kuwataka viongozi hao kuhakikisha kila mtoto anapata chanjo na kukamilisha ratiba.

"Mwaka 2022/2023 kulitokea mlipuko wa ugonjwa wa surua nchini na mkoa wa Tabora pamoja na halmashauri zake ziliathirika na huku zaidi ya watu 5,900 walikiugua sawa na zaidi ya asilimia 50 hivyo lazima tuhakikishe suala hili halijirudii," alisema Mtondoo.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Rufani Kitete mkoani Tabora, Dk. Honoratha Rutatinisibwa, alisema kampeni hiyo inalenga kuongeza kinga kwa watoto wote chini ya miaka mitano kwa kuwapatia chanjo hata kama wamekwishapata.

Dk. Rutatinisibwa alisema wamepokea agizo la kusimamia utekelezaji wa kampeni hiyo kutoka serikalini, lengo likiwa ni kuhakikisha watoto wote wanaolengwa wafikiwe na chanjo hiyo ndani ya muda tajwa.

Baadhi ya viongozi na wadau wa afya mkoani hapa waliahidi kufikisha ujumbe huo katika jamii na kushiriki kikamilifu katika utolewaji wa chanjo hiyo ili iwafikie walengwa kwa wakati uliokusudiwa.

Nipashe
TESA
Jumanne Februari 13, 2024
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**Shinyanga inapaa kukomesha mimba utotoni, wasiobadiliki kajifunzeni kwao**



Ukurasa 12

Asasi yaja kiubinadamu kuwalinda waraibu wasinyanyapaliwe, watajuzwa sheria, haki



Ukurasa 13

El-nino, athari za mafuriko Watanzania jifunzeni haya

ELIMU

**NA JULIETH MKIRERI, KIBAHA**

## HAPPINESS FREDY:

# Licha ya kufiwa, hakukata tamaa ni kinara matokeo ya ‘form 4’ 2023

HAPPINESS Fredy (18), ni mmoja wa wahitimu vinara kwa ufaulu katika mtihani wa kidato cha nne mwaka jana, akibeba alama saba na kupata daraja la kwanza.

Amemaliza masomo katika Sekondari ya Tumbi iliyoko Kibaha mkoa wa Pwani, mwaka 2023, akiibuka na ufaulu wa daraja la kwanza na kuwa msichana kinara kwenye matokeo hayo.

Happiness amesoma tasnifu au mchepuo wa sayansi, akivuna alama A kwenye Fizikia, Kemia, Bailojia, Hisabati, Kiingereza na Kiswahili, kadhalika akipata B kwenye masomo ya Historia na Jiografia.

Akiishi Mtaa wa Tanita mjini Kibaha anaanza kidato cha kwanza mwaka 2020 akitokea Shule ya Msingi John Bosco ya Kibaha pia.

“Nilianza kidato cha kwanza kwa pigo la kumpoteza baba yangu mzazi Fredy Godfrey, haikuwa rahisi kukubaliana na hali hiyo na hapo ndipo historia ya maisha magumu ilipoanza kutokana na misuguano ya kifamilia,” anasema.

Anaongeza kuwa baba yake mjasiriamali wa kuuza vinywaji mbalimbali alikuwa nguzo ya familia na mhusika mkuu wa elimu yake na alipofariki maisha yakabadilika.



Happiness Fredy

Anasema mama yake hakuwa mwajiriwa wala mjasiriamali na kwa ujumla alimtegemea mume wake pekee na alipofariki ilikuwa pia ni mtikisiko.

“Kutokana na maisha nyumbani kuwa magumu nikwenda shuleni kwa msaada wa majirani ambao walikuwa wakinunulia sare za shule, kunilipia nauli na mahitaji ya shule.” Anaongeza.

“Mama hakuwa na biashara wala ajira baada ya baba kufariki alianza kutumia cherehani kushona nguo akiweka viraka ambavyo vilimpa vijisenti kidogo vilivyotusaidia kupata chakula tu,” anasema Happiness.

Anaeleza kuwa familia yao iliishi muda mrefu katika mazingira magumu kutokana na kukosa msaada wa wanafamilia waliokuwa wanataka kuwapora mali za baba yao ikiwamo nyumba.

“Uvumilivu ulifika ukingoni baada ya kufika kidato cha tatu mambo yakazidi kuwa magumu nikatoroka nyumbani kwenda kuishi jirani na shuleni, tena karibu ambako nilikuwa nakwenda na kurudi kila siku.”

“Nilitoroka nyumbani baada ya kuona mateso na vurugu za familia zikiendelea nikaenda kuishi sehemu ambayo hakuna aliyenijua. Nikiwa huko nilikwenda kila siku shuleni mpaka nimemaliza kidato cha nne,” anasema Happness, lakini akakataa kuzungumzia eneo hilo.

Mahali alipokuwa anaishi Happiness napo licha ya kwenda shuleni, anasema palimpa wakati mgumu ni gharama za usafiri. Kila siku alilazimika kupanda magari manne na bodaboda kwenda shule na kurudi nyumbani.

**SHIDA BARABARANI**

Amekumbana na vikwazo vingi ikiwamo kunusurika ajali na ushawishi wa wanaume ambavyo vingekatiza masomo yake.

Pamoja na mambo kuwa magumu aliweka malengo ya kutoka nyumbani saa 11 alfajiri kuelekea shuleni na kurudi saa 3:00 usiku, akiazimia kuwahi na bila kukosa kipindi darasani.

Anasema akiwa shuleni mara nyingi alisahau magumu anayopitia, akiwahi kuingia darasani mpaka saa 8:30 na kusoma hadi jioni lakini pia kufanya majadiliano ya masomo na mwenzake.

“Majadiliano yamenijenga, kunipa ushupavu, kujiamini na kuniimarisha katika masomo huku nikiweka lengo la kufaulu ili niendelee na masomo ya juu.”

Anasema matokeo yalipotangazwa yalimpa faraja, furaha na matumaini tena kumsahaulisha magumu aliyokumbana nayo wakati akisoma.

Anaibuka na alama A nane na B mbili na hivyo kumpa nafasi katika Shule ya Tumbi Sekondari kuwa msichana kinara kwenye matokeo ya mtihani wa kidato cha kwanza.

Binti huyu wa kwanza kwenye familia yake ya watoto watatu anaishukuru serikali kwa kujenga shule za kata na kuendelea kugharamia masomo, akieleza kuwa pengine bila kuwapo kwa shule hizo asingesoma.

“Kilichonipa ushindi katika safari hii ni kukubali kuwa serikali inatusaidia, lazima kusoma. Nitumie muda kujifunza, kushauriana na kushirikiana na walimu na wenzangu na kuwa na msukumo wa kutaka kufaulu.”

Pia, anasema aliweka malengo ya kupata daraja la kwanza japo hakuwahi kuwashirikisha wengine lakini pia amekuwa akimtanguliza Mungu katika kila jambo kwani pamoja na misukosuko ya maisha aliyopitia Mungu amemvusha.

“Pamoja na yote hayo nawashukuru walimu wa Tumbi kwa jitihada za kufundisha wakati wote wakiwa karibu na wanafunzi ili kuwaandaa na kuwajenga kimasomo,” anasema na kuongeza kuwa anatamani kuwa daktari bingwa atakayekuwa karibu zaidi na jamii.

**WASICHANA VINARA**

Mkuu wa Sekondari Tumbi Fidelis Haule, anasema wasichana waliofanya mitihani ya kumaliza kidato cha nne mwaka 2023 walikuwa 34.

Kati ya hao waliopata ufaulu wa

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA SABATO KASIKA, BAGAMOYO

# Asasi yaja kiubinadamu kuwalinda waraibu wasinyanyapaliwe, watajuzwa sheria, haki



Baadhi ya wadau wanaoshiriki elimu ya kuwalinda waraibu. **PICHA: SABATO KASIKA**

KUTUMIA dawa za kulevya kunawageuza vijana kuzipenda na kuzitegemea zaidi hivyo kuwa waraibu. Lakini wanaojidunga wengi wanaambukizwa Virusi Vya Ukimwi (VVU) pamoja na homa ya ini hepatitis C.

Hali hiyo, inailazimisha jamii kuwajali, ikibidi kuwatibu na kulinda afya zao badala ya kuwatenga ili kuwaelimishe kuacha matumizi ya dawa.

Hivi karibuni mradi wa kutoa elimu kwa waraibu wa dawa kukabiliana na unyanyapaa, ubaguzi na unyanyasaji unazinduliwa.

Ni katika tano za Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani, ukishirikisha wadau kuanzia watoa huduma za afya na polisi.

Mradi huo, utatoa elimu kwa familia na jamii kuacha kuwanyanyapaa wanaotumia dawa za kulevya ili wajione ni sehemu muhimu ya familia au jamii inayowazunguka.

Waratibu wa mradi huo wa mwaka mmoja, ni shirika lisilo la kiserikali la kuhudumia waraibu wa dawa za kulevya la Life & Hope Rehabilitation Organisation (LHRO), wakiwezeshwa na Mfuko wa U.S. Ambassador Fund for HIV/AIDS Relief (AFHR Grant) and PEPFAR.

Kata zitakazofikiwa na mradi huo kuwa ni Dunda, Magomeni, Nianjema, Kisutu na Kiromo, anasema Mkurugenzi Mtendaji wa LHRO, Al-Karim Bhanji.

Anasema watoa elimu ni madaktari, maofisa ustawi wa jamii, mahakama, polisi, viongozi wa serikali za vijiji, wa dini na waliowahi kutumia dawa hizo na kuacha.

"Elimu hii inalenga kuimarisha kupatikana haki na huduma nyingine za kijamii kupitia msaada wa kisheria na ushirikiano wa watoa huduma, ndio maana wanahusisha wadau mbalimbali kila mmoja atatoa elimu kulingana na taaluma yake," anasema Bhanji.

Anafafanua kuwa mradi unafanyika kata chache kulingana na bajeti hivyo hawawezi kuzifikia kata zote 11 za halmashauri hiyo.

"Tunashukuru Mfuko wa Mabalozi wa Marekani kwa VVU/Relief(AFHR) na PEPFAR kwa msaada wao muhimu, tutapanua wigo wa kutoa elimu katika kata nyingine zilizobaki iwapo tutapata ufadhili zaidi," anasema.

Bhanji anafafanua kuwa kutakuwa na mikutano ya hadhara katika vijiji, huku kila mdau akipewa nafasi kutoa elimu kulingana na taaluma yake ili kuwajengea uelewa waraibu, familia na jamii inayowazunguka.

"Kwa mfano, ustawi wa jamii watahusika na saikolojia, madaktari watatoa elimu kuhusu umuhimu wa kutumia methadone, watu wa mahakama na polisi watatoa elimu kuhusu sheria," anasema.

Anafafanua kuwa waraibu wananyanyapaliwa au wakati mwingine wanajinyanyapaa wenyewe na kwamba katika mazingira hayo, wanatakiwa kuwekwa sawa na mtaalamu wa saikolojia.

"Madaktari watatoa elimu kuhusu matumizi ya methadone, kwani wapo waraibu ambao huanza dozi na kukatisha, wengine hawajajitokeza kutimia dawa hizo, hivyo, elimu kuhusu madhara ya kukatisha dozi au kukataa kuhudhuria kliniki itatolewa," anasema.

Aidha, kwa upande wa sheria, Bhanji anafafanua kuwa wakati mwingine mraibu ambaye ameanza dozi ya methadone anaweza kufanya makosa akakamatwa na polisi na kuwekwa ndani, na kwamba anatakiwa apewe nafasi ya kwenda hospitali kunywa dawa hizo.

"Kumekuwapo na malalamiko kuwa wanaotumia dozi hizo wakikamatwa kwa makosa mbalimbali hushikiliwa na kunyimwa nafasi kwenda kunywa dawa. Kupitia elimu hii inayokwenda kutolewa, kila upande utajua haki zake za kisheria ili kuondoa mkanganyiko," anasema.

Bhanji anafafanua kuwa watu waliowahi kutumia dawa hizo kisha wakaacha, ambao wako kwenye mradi huo, watakuwa na nafasi ya kushuhudia wenzao ubaya wa dawa za kulevya.

"Kwa ujumla ni kwamba kila mdau ambaye anahusika katika mradi huu, atakuwa na sehemu ya kufanya, ili kusadia waraibu, familia na jamii kujua haki za kisheria na wajibu wa kufanya," anasema.

Ofisa wa Ustawi wa Jamii wa Wilaya ya Bagamoyo, Delvina Maleko ambaye ni mtaalamu wa saikolojia anasema ni muhimu familia na jamii kwa kutambua kuwa si sahihi kuwanyanyapaa waraibu.

"Changamoto kubwa wanayokutana nayo ni mtazamo wa watu wengi kuwaona waraibu kama watu wasiofaa katika familia au jamii, jambo ambalo ni hatari kwao, kwani wanaweza kuchukua uamuzi wowote mbaya ikiwamo kujiua kwa kujiona hawathaminiwi," anasema Delvina.

Delvina anasema, elimu kuhusu madhara ya kulevya itasaidia familia kuwa makini na kusaidia kuwaandaa vijana kuwa viongozi bora wa baadaye walioachana na dawa au ambao hawajawahi kutumia.

"Bila kuchukua hatua mbalimbali zikimo hizi za LHRO za kuanzisha mradi wa kutoa elimu tunaweza kuendelea kuwa na vijana wasio na faida kwenye famili na hata katika jamii," anasema.

Anafafanua kuwa tatizo la unyanyapaa na hata uraibu haviwezi kuisha bila kuwapo elimu na kushirikisha wadau mbalimbali.

"Waraibu wanatakiwa kupata elimu sahihi ya kutumia 'methadone', kujua haki zao za sheria na elimu kuhusu athari za dawa za kulevya, familia na jamii pia ni muhimu kuhusika katika elimu hiyo," anasema.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Dk. Kandi Lussingu, anasema elimu kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya ikiimarishwa inaweza kusaidia vijana kuepuka kutumia dawa hizo.

"Vijana wanaoathirika ni Watanzania na ndio taifa la sasa, wasinyanyapaliwe, wasitengwe bali waelimishwe kuacha matumizi ya dawa hizo," anasema Dk. Kandi.

## Licha ya kufiwa, hakukata tamaa ni kinara matokeo ya 'form 4' 2023

**INATOKA UK.11**

daraja la kwanza ni 14, daraja la pili ni 16 wakati daraja la tatu ni watatu na daraja la nne yuko mmoja akiwasifu kuwa ufaulu wao ni wa juu sawa na asilimia 99.

Haule anasema siri ya ufaulu kwa wasichana hao ni juhudi darasani, nidhamu, kusikiliza walimu pamoja na motisha mbalimbali zinazotolewa na serikali kwa walimu ikiwapo kuwashika mkono na kuwaongezea hamasa ya kazi.

Haule anaongeza: "Namshukuru Makamu wa Rais, Dk.Philip Mpango, Februari 4,2023 alipita shuleni hapo na kutoa motisha ya Shilingi milioni 50 kwa walimu baada ya kuridhishwa na matokeo ya kidato cha nne ya mwaka 2022."

Anasema motisha ya Makamu wa Rais imekuwa chachu ya kuongeza morali kwa walimu katika ufundishaji na kwamba zawadi pekee ilikuwa kuongeza ufaulu.

Haule anasema Tumbi ina vifaa vya kutosha vya kufundishia, walimu pamoja na miundombinu bora iliyokarabatiwa na serikali hivi karibuni.

"Ufaulu huu ni jitihada za serikali maana imefanya kila kitu, kukarabati miundombinu ya shule yetu tunamshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ya kuboresha elimu," anasema Haule.

Diwani wa Kata ya Tumbi (CCM), Raymond Chokala, anasema ufaulu wa wasichana Shule ya Tumbi umetokana na ushirikiano baina ya walimu, wazazi na wanafunzi.

Chokala, anaomba ushirikiano huo uendelee ili shule kinara katika matokeo ya miaka ijayo huku akimpongeza Mkuu wa Shule Haule kusaidia wanafunzi, kushirikiana na walimu kuboresha elimu.

ELIMU

NA DK. FELICIAN B. KILAHAMA

# El-nino, athari za mafuriko Watanzania jifunzeni haya



Mafuriko ndani ya Barabara ya Morogoro eneo la Jangwani ni kikwazo kwa mabasi ya mwendo wa haraka sababu kubwa ni uharibifu wa mazingira na kuchafua Mto Msimbazi. **PICHA: MTANDAO**

WATANZANIA wengi wamekisikia kilio cha athari za mafuriko ya mvua za el- nino za mwaka 2023 kuanzia vifo, uharibifu wa mali kama makazi na mazao na pia kubomoa miundombinu.

Kwa kuangalia mafuriko haya ni vyema kujichunguzwa kujua wapi shida ilipoanzia. Mathalani Dar es Salaam, ulipo Mto Msimbazi kwa miongo takribani minne, kina chake kilikuwa chini na kirefu katika mazingira asilia.

Aidha, hali ya eneo la kandokando ya mto huo ilikuwa ya kuridhisha, maji yalikuwa yanapita na kutiririka bila kukumbana na takangumu wala udongo au mchanga.

Kawaida maji yanapotiririka kwenye mto kutoka ukanda wa juu na kuelekea wa chini, kasi hupungua kadri mto unavyokaribia bahari. Hali halisi ni kwamba sehemu kubwa za udongo, mchanga na takangumu hutua au kugota chini taratibu wakati mto ukiingia baharini au ziwani.

Kadri miaka inavyozidi kupita kina cha Msimbazi na mito ningineyo nchini, huendelea kupungua na kuathiri usafirishaji nyakati za mvua.

Matokeo yake ni 'mafuriko' kutokana na kina cha mto kujaa 'udongo, mchana na takangumu kama inavyoonekana Msimbazi, eneo la Jangwani.

Uzoefu unaonyesha kuwa takribani miongo mitatu iliyopita shughuli za kibinadamu ambazo siyo rafiki kwa mazingira, zimekuwa zikiongezeka wakati miaka ya 1970 na 1980 hali ya vina kwenye mito ilikuwa haijavurugika.

Maji ya mvua yalikuwa yakitiririka kutoka mwanzo wa mito hadi mwisho bila kuzidi au kuharibu kingo za mito wala kujaa udongo, mchanga au takangumu.

Ni kwa mara chache maji yalivuka kingo za mito kutokana na mvua nyingi kupita hali ya kawaida.

Pamoja na hayo, hapajakuwapo na mikakati madhubuti ya kulinda mazingira karibu na mito mfano, wataalamu wa mazingira hawapo vijijini pia mijini ni wachache.

Udhaifu huo ukiunganishwa na wanasiasa kuwa na mitazamo tofauti kuhusu kuhifadhi mazingira, hali kwenye mazingira ya mito ikaendelea kuzorota kila wakati.

Kadhalika, vijiji havina mipango endelevu ya matumizi bora ya ardhi ndani ya mipaka yake na vitongoji vyake, athari sasa zimekuwa kubwa zaidi mathalani, eneo la Mto Msimbazi kwenye barabara ya Morogoro, yapo makatapila yanazotoa tope na takangumu kwenye mto Msimbazi hivyo kutengeneza milima taka kando ya mto.

Ukitafakari kwa undani zaidi, unagundua kuwa huenda yamekosekana maarifa au hakuna kujali ustawi wa mazingira.

Ikumbukwe yanapotokea mafuriko na kupoteza mali wakati mwingine wananchi wanapoteza maisha au ukame ukizidi hadi kusababisha njaa kali, wananchi hulalamikia mabadiliko ya tabianchi kumbe ni binadamu wenyewe ambao wamekuwa wakitekeleza shughuli mbalimbali zisizo rafiki kwa mazingira. Mfano, mataifa tajiri kuendelea kuzalisha hewa ukaa kwa wingi kiasi cha kuathiri ukanda wa ozoni angani na kupelekea ongezeko kubwa la joto duniani.

Wakati huo, nchi zinazoendelea kiuchumi kama Tanzania zinakazani kuinua hali ya maisha ya kila siku na katika harakati hizo uharibifu wa mazingira unazidi kuongezeka kiasi kwamba matokeo yake ni majuto na mahangaiko makubwa kwa raia wengi wa mijini na vijijini.

Kinachojiri kwenye Mto Msimbazi na sehemu nyingine nchini ni kielelezo kwamba kulikuwa na kulijisahau na kufanya mambo kinyume na matarajio chanya.

Ile lugha ambayo ilikuwa inasikika kutoka kwa baadhi ya viongozi wakisema waache wananchi msiwabughudhi, wanaganga njaa, 'wengi wetu sasa "tunaganga-njaa".

Iwapo taifa lingezingatia misingi ya kutunza mito hali isingekuwa kama ilivyo sasa. Serikali isingetumia gharama kubwa aidha kujenga daraja la juu kutoka Magomeni Mapipa mpaka eneo Faya, wala kulazimika kuwahamisha watu waliojenga hadi kingo za Mto Msimbazi.

Maeneo yaliyoonekana kuwa muhimu enzi za wakoloni na ya kahifadhiwa, wakati huo idadi ya Watanzania na mifugo ilikuwa siyo kubwa.

Pamoja na uchache huo, waliona ulazima wa kuyahifadhi kisheria. Baada ya uhuru baadhi ya shughuli zikaanza kuona kuwa hakuna sababu ya msingi kuendelea kuhifadhi.

Watanzania wajiulize maeneo ambayo wakoloni waliyahifadhi kati ya 1930 na 1960 je, walifanya hivyo bila sababu za msingi?

Kwa ujumla, mengi ya maeneo yaliyohifadhiwa ni muhimu mno kwa mustakabali mzima wa taifa na Watanzania kwa ujumla.

Kwanza, yamesheheni uoto asili unaosaidia kuhifadhi vyanzo vya maji misitulindimaji, kadhalika, kwenye maeneo hayo kuna bioanuai au mimea na wanyama, zenye umuhimu mkubwa kimataifa kiasi kwamba baadhi ya mimea na wanyama hupatikana kwenye maeneo hayo Tanzania tu na si kwingineko duniani.

Pili, ni maeneo yenye umuhimu wa pekee kwa kuhifadhi ardhi na uotoasilia ili kuzuia mmomonyoko wa udongo hivyo kuepuka makorongo makubwa kama hali ilivyokuwa eneo la Haubi, wilayani Kondoa Mkoa wa Dodoma baada ya kupata uhuru mwishoni mwa 1961.

Kuna usemi yaliyopita sindwele, tugange yajayo, sasa Watanzania wapo 'njiapanda' mazingira sehemu mbalimbali vijijini na mijini yamejeruhiwa kwa kiasi kikubwa.

Katika maeneo yaliyohifadhiwa kisheria nako huko hali sishwari. Hifadhi kadhaa za misitu hasa misitu ya uzalishaji mazao ya misitu yanazotakiwa kwa maendeleo ya taifa, zimegeuzwa "mashamba ya bibi" ambako kila mtu anafanya anavyotaka na usimamizi wake umelegalega mno.

Hali inatia moyo wenye misitulindimaji au yenye umuhimu mkubwa kimataifa angalau huko usimamizi umeimarishwa.

Watanzania mijini na vijijini, wajitathmini ipasavyo, walipotoka nini visababishi na wajue njia sahihi ya kuondoa vikwazo ili mazingira kwa ujumlawake yasiendelee kuharibika na kusababisha madhara makubwa nchini mathalani, mafuriko kutokana na El-Nino Novemba, 2023.

Vilevile, wajiulize nini kifanyike? Wataalamu waongezewe nguvu hasa wanapojithadi kuhakikisha mazingira, yanatunzwa kwa faida ya wote. Mipango yote kuanzia vijijini hadi taifa, mipango ya maendeleo muda mfupi na mrefu vizingatie umuhimu wa kutunza na kuendeleza mazingira. Shughuli za binadamu zisisababishe kuharibu vyanzo asilia vya maji, misitu ya asili na mapori vilindwe hasa kama maeneo yaliyohifadhiwa kisheria.

Vijiji vitenge maeneo yenye halibora ya misitu na kuyahifadhi kisheri hususani kupitia mipango ya vijiji kwa matumizi bora ya ardhi, kwa kuzingatia Sheria ya Ardhi Vijijini na Kanuni zake na Sheria ya Misitu.

Shughuli za ugani na elimu ya mazingira kwa wananchi ziimarishwe na wataalamu wawezeshwe ipasavyo ili huduma za ugani, ufuatiliaji na uperembaji zifanyike, kutekelezwa ipasavyo.

Vilevile, kuwepo na ushirikiano kitaaluma mfano, kilimo, mifugo, umwagiliaji, misitu, ufugaji-nyuki, wanyamapori, uvuvi, maendeleo ya jamii, biashara na viwanda na wengineo.

Wataalamu wa fani za, uhasibu, mipango, ukaguzi na manunuzi, ugavi ni maeneo mtambuka hivyo wanafaa kwenye makundi mbalimbali ya kitaaluma. Nia iwe ni kujenga mshikamano katika kuiwezesha serikali kufanya maamuzi sahihi kwa kujikita zaidi kwenye misingi ya kitaaluma.

Naamini kukiwapo mshikamano kati ya viongozi, wataalamu na wananchi taifa litapiga hatua kubwa katika kujiletea maendeleo endelevu.

Roho za ubinafsi na kutowajibika ipasavyo hazitapata nafasi, lengo kuu liwe kuimarisha na kuendeleza maishabora kwa Watanzania wote pamoja na kuwahakikishia kuwa usalama wa chakula na lishe, umoja wa kitaifa na amani.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Shinyanga inapaa kukomesha mimba utotoni, wasiobadiliki kajifunzeni kwao



Wanafunzi wanahitaji kulindwa ili wasichana na wavulana wawe na haki sawa za kielimu. **PICHA: MTANDAO**

TAZAMA maisha ya mabinti mkoani Shinyanga, mmoja ameachishwa shule ili aozwe wazazi au walezi wavune mali ambayo ni mahari inayohusisha mifugo na fedha. Yuko, anayelazimishwa kuandika majibu ya uongo kwenye mitihani ili asifaulu, ni mbinu ya kumwandaa kuozwa.

Wakati wenzao hao, wazazi na walezi wao wanawasakia wachumba kwa kuwalazimisha kuacha shule na kujifelisha mitihani, yote hayo yakiwatoa darasani, wapo mabinti ambao wamepata mimba utotoni wakiwa machungani kuwalisha ndama wa ng'ombe, mbuzi na kondoo.

Hayo yanajiri katika mkoa wa Shinyaga, ambao hali ya mimba za utotoni leo imepungua, kwa mujibu wa takwimu zinazotolewa na Tanzania Demographic Health Survey (TDHS) mwaka 2022.

Tatizo hilo limepunguzwa kutoka asilimia 34 hadi 21, TDHS inasema, maelezo yanayokuja muongo mmoja baada ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), kuutangaza kuwa ni wa kwanza kwenye mimba na ndoa za utotoni kitaifa.

Mwaka 2012 utafiti wa UNCEF ulibaini kuwa Shinyanga ndiyo kinara ndoa za utotoni kwa asilimia 59 ikimaanisha kuwa katika mabinti 100 wanaozwa ni 59 kadhalika na mimba katika idadi hiyo 34 hukutwa na mimba ikumbukwe ni watoto wa chini ya miaka 18.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Shinyanga, Lidya Kwesigabo, anasema kitu ambacho kimechangia kupunguza tatizo la mimba za utotoni ni kutoa elimu ya ulinzi wa mtoto kwa jamii nayo ikahamasika, pamoja na kuwachukulia hatua kali wanaume ambao huwapatia ujauzito watoto ikiwamo kifungo jela.

Anasema wameipatia jamii elimu ya ulinzi kwa mtoto kwa kushirikiana na wadau wakiwamo mashirika mbalimbali ya kijamii ili kutambua kwamba ulinzi wa mtoto ni jukumu la kila mtu kuanzia mzazi, mlezi, mwalimu, kiongozi wa dini na jamii nzima kwa mujibu wa sheria ya mtoto ya mwaka 2009, hali ambayo imechangia kuzipungua.

Anaeleza kwamba awali jamii haikuwa na elimu ya ulinzi wa mtoto, na ndiyo maana watu walipoona mtoto akifanyiwa vitendo vya ukatili hawakutoa taarifa kwa kuogopa lawama, lakini baada ya elimu wanaripoti na watuhumiwa kukamatwa.

"Elimu ya ulinzi wa mtoto ngazi ya jamii, kuunda mabaraza ya watoto, wanafunzi kuhamasika na kujitambua pamoja na kuwafunga jela washtakiwa kupunguza tatizo la mimba za utotoni Shinyanga," anaongeza Lydia.

"Tulidhibiti tatizo la kuharibu ushahidi kwa kuhifadhi wahanga wa mimba za utotoni katika makao ya watoto, ili wasirudi majumbani na kuharibu ushahidi kwa kuwakana watuhumiwa ambao wamewapatia ujauzito baada ya wazazi wao kupewa hongo na wahusika," anaongeza Lydia.

## KUTOKOMEZA MIMBA

Ofisa Ustawi wa Jamii anaahidi kuwa serikali itaendelea kushirikiana na wadau kutoa elimu ya ulinzi wa mtoto kwa wazazi na walezi pamoja na kuwapatia wanafunzi elimu ya kujitambua wakihusisha mashirika yanayotekeleza miradi ya utetezi wa haki za watoto.

Anasema muongozo umeshatolewa kwa shule zote za serikali na binafsi, kuwepo na dawati la kukusanya maoni taarifa za ukatili na kisha kufanyiwa kazi na wahusika kuchukuliwa hatua ili kudhibiti ukatili dhidi ya watoto zikiwamo mimba na ndoa za utotoni.

Dedan Rutazika ni Ofisa Elimu ya Watu Wazima Mkoa wa Shinyanga, anasema wana mkakati wa kutekeleza maelekezo ya serikali ya kusomesha mabinti ambao walikatishwa masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo ujauzito, wanaopewa elimu ya watu wazima.

Kupitia Mradi wa Kubopresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP), kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, wameweka mkakati wa kusaidia mabinti ambao walikatiza masomo wakiwamo waliopata ujauzito.

"Vituo vya kutoa elimu kwa mabinti hawa vimeshatengwa, kikiwamo cha Sekondari Huru, Gembe, Solwa, Kishimba, Shule ya Msingi Nhelegani, na Kituo cha BSL Open School, wanachopaswa kufanya ni kwenda kujiandikisha na hakuna cha kulipia," anasema Rutazika.

## DAWATI LA JINSIA

Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga, Victoria Maro, anasema imekuwa na mwamko wa kutoa taarifa za ukatili dhidi ya watoto na watuhumiwa wamekuwa wakiwatia nguvuni wakiwamo waliowapatia ujauzito wanafunzi na kuwachukulia hatua kali za kisheria.

Anataja takwimu za matukio ya ukatili katika mkoa wa Shinyanga kwa mwaka jana ambayo yalitolewa taarifa, kuwa ni 51 zikiwamo mimba za utotoni, ambapo wahusika walifikishwa mahakamani na wengine kuhukumiwa vifungo jela.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2008 inasema anayempa ujauzito mwanafunzi kifungo chake ni miaka 30 jela.

## OFISI YA MASHTAKA

Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Mashitaka Mkoa wa Shinyanga Ajuaye Zegeli, anataja takwimu za kesi za mimba za utotoni katika wilaya ya Shinyanga, kwamba mwaka jana zilikuwa 22 na kwamba 20 zilishatolewa maamuzi, ambapo wanaume 12 wamefungwa miaka 30 na washitakiwa sita waliachiwa huru baada ya kukosa ushahidi na kesi mbili bado zinaendelea mahakamani.

Ofisa Mradi wa Shirika la Mfuko wa Ruzuku wa Wanawake na Watoto (WFT-Trust) Mkoa wa Shinyanga, unaohusika na utetezi wa haki za wanawake na watoto, Glory Mbia, anasema wamewezesha mkoa huo kwa zaidi ya miaka mine.

Wakitekeleza mpango mkakati wa kukomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA), na kufurahia matokeo chanya ya kupungua mimba utotoni.

Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 kifungu cha 13 kinaruhusu mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 14 kuolewa kwa ridhaa ya mahakama, huku mtoto mwenye umri wa miaka 15 anaruhusiwa kufunga ndoa kwa ridhaa ya wazazi.

Hata hivyo, Mahakama Kuu imeitaka serikali kurekebisha vifungo hivyo, japo hukumu haijetekelezwa.

Mkurugenzi wa Shirika la Thubutu Afrika Intiatives, Jonathan Manyama, lenye miradi ya utetezi wa haki wanawake na watoto mkoani Shinyanga, anasema kutolewa elimu kwa wananchi kumekuwa na mchango mkubwa kupunguza tatizo la mimba za utotoni.

Anasema elimu ni kitu cha msingi kubadilisha jamii juu ya kuondokana na tatizo la ukatili dhidi ya watoto, ndiyo maana shirika lao limejikita zaidi kuwapatia uelewa wananchi, pamoja na watoto wa kike kujitambua ili wasijiingize kwenye mahusiano.

Mzazi Mabula Manyanda, anasema elimu zaidi inahitajika kwa wazazi na walezi vijijini ili kuachana na mila kandamizi za kumuoza binti badala ya kumsomesha



# BRELA kurekebisha sheria ya kampuni

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

WAKALA Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) umejipanga kuanza mchakato wa kurekebisha sheria ya kampuni, ili kuondoa vikwazo katika mazingira ya biashara.

Mtendaji Mkuu wa BRELA, Godfrey Nyaisa, alitoa kauli hiyo jana wakati wa semina ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo, Mifugo na Uvuvi ilipokuwa ikipokea taarifa ya utendaji kazi wa wakala huo jijini hapa.

Alisema maboresho ya sheria hiyo ni utekelezaji wa azma ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuweka mazingira mazuri ya biashara nchini.

"Tumewaeleza wabunge tunakwenda kupitia sheria ya kampuni ambayo ni ya zamani, ili kwenda na wakati katika kuhudumia Watanzania na kuhakikisha biashara za Watanzania zinakua badala ya kuwa na sheria zinazoleta makwazo," amesema. Aidha, alisema mwaka 2018 BRELA ilianza kutumia mifumo ambayo inawezesha Watanzania kusajili kampuni kwa njia ya mtandao.

Mwenyekiti wa kamati hiyo ya Bunge, Deo Mwanyika, aliseme wameridhishwa na utendaji kazi wa BRELA na kusisitiza kuwa ni muhimu wabunge kuwa na ufahamu wa taasisi hiyo, ili kuisimamia na kufikia azma ya Rais Samia kwa kuwa serikali imefanya mageuzi makubwa BRELA.

"Mazingira haya mazuri ya biashara ni kwa wawekezaji wa ndani na nje sasa taasisi hii ndio uhai wa mazingira ya biashara, dirisha la kwanza ambalo mwekezaji anakutana nalo ni BRELA tunawapongeza sana zile kazia ambazo walikuwa wanapata wawekezaji kwa sasa zimepungua sana," alisema.

Mwanyika alisema hali hiyo itaiweka Tanzania kuwa nchi yenye mazingira mazuri ya uwekezaji na kuwaasa wajipange kuwalea wafanyabiashara kupitia maofisa biashara ya halmashauri. Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaudi Kigahe, alisema serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji nchini.



Wabunge wakiwa wamesimama bungeni jijini Dodoma ikiwa ni ishara ya kuombeleza kifo cha Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa kilichotokea Februari 10 mwaka huu, taarifa hiyo iliwasilishwa bungeni na Naibu Spika, Musa Zungu.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Walimu awali, la kwanza wanolewa mitaala mipya

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WALIMU 639 wanaofundisha darasa la awali na la kwanza katika shule za mkoani Singida wameanza kupewa mafunzo ya uimarishaji wa ufundishaji na ujifunzaji.

Mafunzo hayo yameandaliwa na Taasisi ya Elimu Tanzania kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa ufadhili wa Programu ya Shule Bora. Mratibu wa Programu ya Shule Bora wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Winifrid Chilumba, akizungumza jana alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo walimu wa ngazi hizo ili waendane na mitaala mipya.

"Katika mafunzo haya walimu tumewasisitizia umahiri sahihi katika maeneo katika ufundishaji somo la kiingereza ambalo tunataka wanafunzi wajue kusoma, kuandika na kuhesabu, eneo jingine ni la ujumuishi na matumizi ya TEHAMA," alisema. Chilumba alisema TAMISEMI inatarajia walimu wanaofundisha madarasa hayo wataweza kupata stadi zinazotakiwa ili kuendana na matakwa ya mitaala mipya.

"Matokeo tunayoyatarajia ni kuona wanafunzi wanajua kusoma, kuandika na kuhesabu na pia wanakuwa na uwezo wa kumudu somo la Kiingereza hasa eneo la kuzungumza," alisema.

Mratibu Elimu Jumuishi, Emmanuel Stanslaus, alisema wameandaliwa walimu watakaokuwa wawezeshaji kitaifa namna ya kuwabaini wanafunzi wenye mahitaji maalum na namna ya kuwasaidia kwa njia stahiki.

# Wabunge wataka NHIF kuongeza ubunifu utoaji elimu kwa umma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI imeutaka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kuongeza ufanisi na ubunifu wa kutoa elimu kwa wananchi kujiunga na bima ya afya.

Hali ambayo itasaidia kuongeza idadi ya wanachama wengi watakaochangia na kufanya mfuko kuwa endelevu na kutoa huduma zake kwa ufanisi mkubwa. Ushauri huo ulitolewa juzi jijini hapa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, Stanslaus Nyongo baada ya kupokea taarifa ya hali ya utendaji na majukumu ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

Nyongo alisema kuna haja ya kusogeza elimu kwa wananchi waliopo katika ngazi ya msingi, ili kuwa na uelewa na umuhimu wa bima ya afya kabla ya kuanza kutekeleza sheria ya bima ya afya kwa wote.

"Nina imani kubwa mkifanikiwa katika kutoa elimu kwa jamii ya ngazi ya msingi sheria ya bima ya afya kwa wote, ikianza kutekelezwa wananchi watakuwa tayari wana uelewa juu ya kuwa na bima ya afya," alisisitiza Nyongo.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dk. Faustine Ndugulile, alitoa wito kwa uongozi wa NHIF pamoja na Wizara ya Afya kufanya tafiti mbalimbali juu ya uendeshaji wa mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili kupata ujuzi namna ya kuendesha wakati sheria ya bima ya afya kwa wote itakapoanza kutumika.

# DC aagiza elimu kuhusu lishe, bima ya afya iliyoboreshwa

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MANYONI

MKUU wa Wilaya ya Mkalama, Moses Machali, amewaagiza watendaji wa kata, watumishi wa afya na wahudumu ngazi ya jamii kuhakikisha wanatoa elimu kwa jamii kuhusu lishe pamoja na bima afya iliyoboreshwa.

Ametoa agizo hilo juzi katika kikao cha tathimni ya lishe kwa kipindi cha robo ya pili ya mwaka wa fedha 2023/2024.

Machali alisema kila mmoja kwa nafasi yake atimize wajibu wake kikamilifu katika kutoa elimu ya lishe kwa jamii pamoja na kutembelea watoto chini ya miaka mitano, kinamama wajawazito ili watambue umuhimu wa lishe.

Alisema wazazi pia waelimishwe kuhusu kuendelea kuchangia chakula shuleni, ili kutengeneza taifa la watoto wenye afya bora na wenye utimamu wa akili.

"Jitumeni, tusifanye kazi kwa kuvutana suala la lishe ni ajenda ya taifa hakikisheni mnakwenda kutoa elimu kwa wananchi, ili waweze kufahamu suala la lishe sahihi, tamko la jiongeze tuwavushe salama pamoja na bima ya afya iliyoboreshwa,"alisema.

Mkuu huyo wa wilaya pia aliwaagiza kuhakikisha wanasimamia vizuri mapato ya hospitali, vituo vya afya na zahanati na kuwataka kujenga utamaduni wa kutembelea maeneo ya kutokea huduma za afya kujua idadi ya wagonjwa waliopatiwa huduma katika vituo vinavyohusika, ili pesa inayopatikana kutokana na matibabu hayo ziweze kutatua changamoto mbalimbali zilizopo kulingana na ufinyu wa bajeti.

Awali, akiwasilisha taarifa ya hali ya lishe, Ofisa Lishe Wilaya ya Mkalama, Zacharia Nyahende, alisema halmashauri imejiwekea vipaumbele kwa mwaka 2023/2024 kuwa ni kuhakikisha kitengo cha lishe kinaendelea kuimarisha huduma za lishe hususani kwa watoto chini ya miaka mitano, vijana balehe, wanawake wenye umri wa kuzaa pamoja na wazee.

Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto, Emmanuel Ngeleja, alisema kuwa wilaya inaendelea kuimarisha mfumo wa M-Mama katika maeneo yote ndani ya wilaya, ili kumsaidia mama na mtoto na kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuchukua hatua za mapema kwa mama anapojihisi uchungu hasa akiwa nyumbani.

Alisema zimeundwa kamati zinazohusika kufuatilia wajawazito pamoja na kuendelea kuhimiza kinamama kupata huduma ya 'Ultrasound' kwa kipindi cha ujauzito ili kubaini changamoto mapema na kuzifanyia kazi.





# MSD yatoa tuzo halmashauri tatu kwa ulipaji fedha mzuri

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BOHARI ya Dawa (MSD) Kanda ya Mbeya imetoa tuzo maalum kwa halmashauri tatu kati ya 19 za mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kutokana na kulipa fedha zote za manunuzi ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi ambavyo bohari hiyo ilizisambazia katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Halmashauri hizo ambazo zimetajwa kuwa hazina deni lolote la dawa, vifaa tiba wala vitendanishi kutoka MSD ni Ileje na Tunduma zilizopo mkoani Songwe na Bosokelo ya mkoani Mbeya.

Tuzo hizo zilikabidhiwa kwa waganga wakuu wa halmashauri hizo mwishoni mwa wiki, wakati wa kikao cha wadau wa MSD kilichokuwa na lengo la kujadili utekelezaji wa majukumu ya taasisi hiyo na namna ya kutatua kero zinazoikabili na wadau wake.

Meneja wa MSD Kanda ya Mbeya, Marco Masala, alisema kanda hiyo inahudumiwa halmashauri zote za mikoa ya Mbeya, Songwe, Rukwa na Halmashauri ya Makete mkoani Njombe pamoja na Hospitali za mikoa hiyo na Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya.

Alisema halmashauri hizo zilitumia vyanzo vingine kulipa fedha hizo bila kutegemea bajeti ya serikali kuu na kwamba waliamua kuzikabidhi tuzo hizo kama sehemu ya kutambua mchango wao na kuhamasisha halmashauri zingine.

"Tuzo hizi ni sehemu ya hamasa kwa waganga wakuu wa mikoa na wilaya kusimamia vema vyanzo vya mapato ili fedha wanazokusanya wazitumie kununua dawa na vifaa tiba kwa ajili ya vituo vyao vya kutolea huduma, lakini mbali na tuzo hizi pia tumetoa vyeti kwa wateja wetu wote," alisema Masalala.

Hata hivyo, alisema kutokana na ongezeko la vituo vya afya katika mikoa hiyo, wamejipanga kuongeza ufanisi kwa kushirikiana na wadau pamoja na wateja wanaowahudumia huku akidai kuwa kikao hicho ni moja ya mikakati ya uboreshaji wa huduma.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Enock Mwambalaswa, alisema halmashauri hiyo imekuwa ikikusanya mapato kwenye vituo vyake vyote kwa kufuata miongozo na kanuni mbalimbali ya serikali.

Alisema wamekuwa wakikusanya fedha ambazo wananchi wanachangia papo kwa papo, kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na Bima ya Afya ya Jamii iliyoboreshwa (ICHF) na kuzitumia kununulia dawa na vifaa tiba pamoja na kulipa madeni.

"Lakini sisi tumekuwa tukiagiza dawa kila baada ya miezi mitatu, tumekuwa tukiagiza kwa wakati na kulipa malipo yote tunayotakiwa kulipa kwa wakati," alisema Mwambalaswa.

Alisema tuzo waliyoipata itawafanya waongeze juhudi katika kutumia mapato ya ndani kununua dawa na kulipa madeni wanayodaiwa na bohari hiyo.

Akifungua mkutano huo, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, aliwataka wadau wote wa MSD kutekeleza majukumu mbalimbali yanayowakabili kwa weledi ili kuwahudumia vizuri wananchi na kupunguza manung'uniko.

Aliwataka wadau wote wa bohari hiyo kufanya maoteo ya bidhaa za afya kwa usahihi na kwa wakati kwa maelezo kuwa utaratibu huo utaiwezesha MSD kuwa na takwimu sahihi kuagiza bidhaa hizo kutoka kwa wazalishaji.



Maofisa wa vyombo vya ulinzi na usalama mkoani Mbeya wakishiriki kikao cha Kamati ya Ushauri ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kilichofanyika mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Viongozi wa mila washauri h'shauri kujenga vyoo uwanja wa mikutano

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa mila mkoani Mbeya, wameshauri Halmashauri ya Jiji la Mbeya, kujenga vyoo katika Uwanja wa Shule ya Msingi Kagera ambapo mikutano ya hadhara imekuwa ikifanyika, ili kupunguza uchafuzi wa mazingira.

Mwenyekiti wa machifu wa Jiji la Mbeya, Rocket Mwashinga, alisema watu ambao wamekuwa wakifanya mikutano kwenye uwanja huo wamekuwa wakitumia vyoo vya shule na hivyo kusababisha uchafuzi wa mazingira.

Alisema baadhi ya watu wamekuwa wakijisaidia pembezoni mwa uwanja huo na kwenye mapagara hali ambayo inasababisha uchafuzi wa mazingira.

Chifu Mwashinga alisema endapo serikali itajenga vyoo kwenye eneo hilo kutapunguza uchafuzi wa mazingira na kuepuka watu wazima kuchangia vyoo vya shule.

"Lile eneo linafanyika mikutano kila wiki na huwa inakusanya watu wengi, mingine inakuwa ya dini na mingine ya kisiasa, sasa ule utaratibu wa kutumia vyoo vya shule haufai kabisa ndio maana tunashauri vijengwe vyoo," alisema Mwashinga.

Alisema kitendo cha watu wazima kutumia vyoo vya shule kwenye mkusanyiko mkubwa kunaweza kukasababisha kusambaa kwa baadhi ya magonjwa kwa wanafunzi.

Akijibu ombi hilo, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alisema watalifanyia kazi kulingana na bajeti kwa maelezo kuwa eneo hilo linakusanya watu wengi.

# Mil. 300/- kukamilisha ujenzi zahanati sita Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

ZAIDI ya Sh. milioni 300 zinatarajiwa kutumika kukamilisha ujenzi wa zahanati sita katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Mkoa wa Njombe kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Valentino Hongoli, katika wa uzinduzi wa kikao cha robo ya pili ya mwaka.

Hongoli alisema zahanati hizo ni kwa yale maeneo ambayo yamekosa vituo vya kutolea huduma za afya.

"Hizi zahanati zilizotajwa kama mtaalamu alivyosema kwamba ni kwa maeneo ambayo hayana huduma za afya zaidi za hizo zinazotarajiwa kuanzishwa tukikamilisha miradi hiyo," alisema Hongoli.

Hata hivyo, alisema kukamilika kwa zahanati hizo kutasaidia wananchi kuacha kutembea umbali mrefu kwenda kutafuta matibabu.

Katibu wa Afya wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Domina Kusuva, alisema tayari bajeti imeshatengwa ya kwenda kukamilisha ujenzi wa zahanati hizo. "Hizo zahanati sita zinaendelea na ujenzi katika mwaka wa bajeti 2023/24 hivyo vituo vyote vinahela ambazo zinaenda kukamilisha, lakini mwongozo wa fedha za vifaa tiba unaoletwa si kwa ajili ya vituo vinavyoendelea lakini ni kwa ajili ya vituo ambavyo vimemaliza ujenzi," alisema Kusuva.

Ofisa Mipango Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Lwidiko Mella, alisema kiasi cha Sh. bilioni 33.6, ikiwa mapato ya ndani Sh. bilioni 4.1 zinatarajiwa kwenda kupunguza changamoto katika miradi hiyo viporo inayolalamikiwa kwa muda mrefu ukiwamo wa Kituo cha Afya Mtwango.

"Vipaumbele vilivyojadiliwa ni pamoja na miradi viporo, tuna miradi mingi katika meneo yetu lakini kutokana na uhaba wa rasilimali fedha haikuweza kukamilika," alisema Mella.

Katibu Tawala Wilaya ya Njombe, Agatha Mhaiki, anasisitiza suala la usafi ili kujikinga na magonjwa ya mlipuko na ya kuambukizwa.

"Nitoe tahadhari kuhusu kipundupindu pamoja na ugonjwa wa macho ambao sasa hivi unasambaa nchini, jirani zetu wamepata hili tatizo na mzunguuko wa watu upo na unaweza ukasambaa kwa hiyo tuchukue tahadhari tuhimizane kwamba tuoshe mikono, tuoshe nyuso zetu na kutumia kinga za macho na mikono," alisema Mhaiki.





# Maswali 181 kutikisa Baraza la Wawakilishi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUTANO wa 14 wa Baraza la Kumi la Wawakilishi Zanzibar unatarajiwa kuanza kesho, ambapo kutakuwa na shughuli mbalimbali ikiwamo maswali na majibu 181.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake Chukwani nje ya mji wa Zanzibar, Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Raya Issa Msellem, alisema katika kikao hicho pia kutakuwa na uwasilishwaji wa ripoti za kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2023/2024.

Aidha, alisema katika mkutano huo pia miswada miwili ya sheria itawasilishwa na ambayo ilisomwa kwa mara ya kwanza katika mkutano uliopita na sasa itasomwa kwa mara ya pili na kujadiliwa katika kikao hicho.

Alitaja miswada hiyo ni muswada wa sheria ya kufuta Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar namba 12 ya 2019 na kutunga Sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar kusimamia huduma za serikali mtandao Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Alisema mswada mwingine ni wa sheria ya kufuta Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar, namba tatu ya mwaka 2011 na kutunga Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar kwa ajili ya kutoa msaada wa kifedha wa wanafunzi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Katibu huyo wa baraza alisema pia kutawasilishwa taarifa ya wabunge watano wanaoliwakilisha Baraza la Wawakilishi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Hata hivyo, alisema katika kikao hicho, kutawasilishwa ripoti ya mapendekezo ya mwelekeo wa mpango wa Taifa na ripoti ya utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) kwa mwaka 2020/2021.

"Ripoti ya Mwaka ya Mamlaka ya Dawa za Kulevya, Zanzibar ya mwaka 2022/2023 nayo itawasilishwa katika kikao hiki," alibainisha katibu huyo.




Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao cha Halmashauri Kuu ya chama hicho chenye lengo la kufanya maandalizi ya mkutano mkuu Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# JKU: Hakuna ajira mpya kwa vijana

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU) umesema hakuna ajira mpya zinazotolewa kwa vijana kujiunga na jeshi hilo na mchakato unaoendelea kwa sasa ni utaratibu wa kawaida wa kusajili vijana kwa ajili ya kujiunga na mafunzo ya kila mwaka ya jeshi hilo kwa mujibu wa sheria.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), Kanali Makame Abdalla Daima, wakati akizungumza na waandishi wa habari visiwani humo, kuhusu taarifa kwamba jeshi hilo limeanza kutoa ajira kwa vijana na kusababisha taharuki kwa watu kufuatilia nafasi hizo.

Alisema habari zinazozagaa mitaani kwamba jeshi hilo limeanza kutoa ajira kwa vijana sio za kweli na upo utaratibu wa kutoa ajira kwa mujibu wa sheria unaofanyika.

Aidha, alisema kwa sasa jeshi la kujenga uchumi linafanya usaili wa vijana wanaotaka kujiunga na jeshi hilo kwa mujibu wa sheria. Kanali Daima alisema jeshi la kujenga uchumi tangu kuanzishwa kwake linapima na kuchukuwa vijana kwa ajili ya kujenga taifa kwa ajili ya kuwapatia mafunzo ya kuwajenga uzalendo na stadi za maisha kwa ajili ya kazi mbalimbali za mikono.

Alisema mafunzo hayo huwapatia vijana vyeti ambavyo ni miongoni mwa vigezo vyake ni wakati wa kuomba ajira katika sekta mbalimbali serikali au katika vyombo vya ulinzi na usalama. Kanali Daima aliwataka wananchi kufahamu kwamba mfumo wa ajira katika idara maalum SMZ upo kwa mujibu wa sheria zinazoongoza idara maalum za serikali ya mapinduzi ya Zanzibar chini ya Tume ya utumishi ya idara maalum SMZ.

Aidha, aliwataka wananchi ikiwamo wazazi kupuuza uvumi huo ambao unaweza kutumiwa vibaya na watu wachache kwa ajili ya kujipatia fedha na kujinufaisha binafsi.

"Huu ni uzushi na utapeli ambao unaweza kutumiwa na watu wachache kwa ajili ya kujipatia fedha kwa njia ambazo sio halali...ajira za serikali na Idara maalumu utaratibu wake unafahamika na upo kwa mujibu wa sheria," alisema.

Baadhi ya wananchi wamelipongeza Jeshi la Kujenga Uchumi kwa ufafanuzi wake kwa sababu tayari baadhi ya watu "matapeli" walianza kutumia fursa hiyo kwa ajili ya kujinufaisha na kuomba fedha za kuwatafutia ajira katika idara maalum SMZ.

"Mimi nilifuatwa na watu wakiniambia ajira tayari zinatolewa katika vikosi vya idara maalum SMZ kwa hivyo nitayarishe fedha," alisema Khamis Haji mkazi wa visiwa hivyo.

# Zanzibar yataja sababu kupaa bei ya mafuta

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KUONGEZEKA kwa bei za mafuta katika soko la dunia kumesababisha kuchangia bei ya mafuta ya petroli kupaa visiwani Zanzibar kwa mwezi huu.

Akitangaza mabadiliko ya bei za mafuta mwishoni mwa wiki ofisini kwake Maisara visiwani humo, Meneja wa Kitengo cha Uhusiano wa Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Mbarak Hassan Haji, alisema ZURA hupanga bei za mafuta kwa kuzingatia wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la dunia.

Alisema kwa mwezi huu mafuta ya petroli yamepanda kwa wastani wa asilimia 1.38 ambapo kwa lita moja yanauzwa kwa Sh. 2,933 ikilinganishwa na mwezi wa Januari ambayo yaliuzwa kwa Sh. 2,893 ni tofauti ya shilingi 40.

Alisema mafuta ya dizeli nayo yamepanda bei ambapo kwa mwezi huu yanauzwa kwa Sh. 3,102 ikilinganishwa na Januari ambayo yaliuzwa Sh. 3,101.


Aidha, alisema sababu nyingine ya kupanda kwa bei hizo ni gharama za uingizaji mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam na Tanga, thamani ya shilingi ya dola za Kimarekani, gharama za usafiri, bima na 'premium' hadi Zanzibar.

"Pia sababu nyingine ni kodi na tozo za serikali na kiwango cha faida kwa wauzaji wa jumla na rejareja," alifafanua meneja huyo.

Kuhusu bei ya mafuta ya ndege imeshuka kutoka Sh. 2,825 kwa mwezi uliopita na mwezi huu yanauzwa kwa Sh.2,636 sawa na asilimia 6.69 tofauti ya Sh.189.

Akitaja sababu ya kushuka kwa bei hiyo, meneja huyo alisema ni kupunguwa kwa gharama za mafuta hayo katika soko la dunia.

Hata hivyo, alisema bei ya mafuta ya taa itabaki kuuzwa ile ya mwezi uliopita wa Januari ambayo ni 3,200 huku akiwataka wananchi kununua mafuta katika vituo halali vya mafuta na kudai risiti za kielektroniki kila wanaponunua mafuta.



Mbunge wa Jimbo la Mikumi, Denis Lazaro Londo (kushoto), akikabidhi funguo kwa Daktari Kiongozi wa Kituo cha Afya, Malolo Yohana, baada ya kuwapatia gari la wagonjwa ili kuwasaidia kwa usafiri na kuwaepusha na vifo visivyotarajiwa. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

# Wafichua siri wagonjwa kifafa kukimbilia nyumba za ibada

**Na Mary Geofrey**

IMANI potofu kuhusu ugonjwa wa kifafa ndio sababu kuu ya wagonjwa wengi wenye tatizo hilo kutegemea tiba mbadala kama nyumba za ibada, waganga wa kienyeji, wapigaramli na kupuuza tiba za hospitalini.

Kutokana na wagonjwa wengi kutokwenda hospitalini, wanapoteza maisha kwa kudondoka katika mazingira hatarishi yenye vitu vya ncha kali, maji au moto.

Profesa wa Magonjwa ya Mishipa ya Fahamu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), William Matuja, alisema kifafa ni ugonjwa sugu wa neva ambapo ubongo hufanya kazi kwa njia isiyo ya kawaida na husababisha mshtuko wa mara kwa mara.

Alisema kifafa ni dalili za matatizo ya ubongo ambayo yanaweza kutokea ghafla na kusababisha shughuli ya umeme isiyo ya kawaida katika ubongo, kupoteza fahamu na degedege kwa muda mrefu (mwili hutetemeka bila kudhibitiwa). Inaweza kuathiri watu wa rika zote bila kujali jinsia zao na hata rangi.

Licha ya wataalamu kueleza sababu za ugonjwa huu, bado jamii imekuwa mstari wa mbele kuamini sababu za kishirikina, wagonjwa kupoteza maisha kwa kukosa matibabu sahihi na unyanyapaa unaowafanya wagonjwa wakate tamaa.

Licha ya jitihada zinazofanywa na Wizara ya Afya kutoa tiba sahihi za ugonjwa huu katika vituo vyote vya afya nchini, bado uelewa mdogo ni tatizo linalokwamisha juhudi hizo.

Katika kuadhimisha Siku ya Ugonjwa wa Kifafa Duniani leo, Nipashe inafanya mazungumzo na kijana anayeugua kifafa kwa miaka 12.

Alianza kuanguka kifafa akiwa na miaka 13, alianza matibabu akiwa na miaka 21 na kufanikiwa kukata minyororo ya kunyanyapaliwa, umaskini na kuwa balozi wa kusaidia wengine kupatiwa matibabu.

Omari Vadenga (25) anasema tangu aanze matibabu, hajaanguka kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa kutoka kuanguka mara tatu kwa siku, amezingatia matibabu na matumizi sahihi ya dawa.

Anasema alifanikiwa kuvifahamu vichocheo vinavyomfanya aanguke kifafa ili kuwahi kuchukua tahadhari na hivyo kumpunguzia madhara kama mejaraha kudhalilika zaidi.

"Bado tatizo kubwa ni uelewa, wagonja wengi wamekata tamaa kwa sababu ya imani walizomezeshwa kutoka kwa watu wanaowazunguka, hawaamini katika matibabu ya hospitalini.

"Kuna siku nilianguka kwenye daladala, nikapata msaada kutoka kwa mdogo wangu wakanirudisha nyumbani, nilipozinduka nikabadili shati kwa sababu lilichafuka sana, nikavaa tisheti ya shule, nilipofika shuleni, nikiwa mstarini nyuma kabisa, alikuja mwalimu akanikata mtama kwa sababu nimevaa shati chafu bila kunipa muda wa kujieleza ilhali wanafahamu nina tatizo la kifafa.

"Huo ulikuwa mwanzo wangu wa kuchukia shule na kutamani kukaa nyumbani kwa sababu nilijiona sistahili tena kuchangamana na wengine wala sina nafasi ya kusikilizwa," anasema.

Anabainisha kuwa aliacha kwenda shuleni lakini nyumbani nako wakaanza kusumbua kwa sababu alikuwa "mzigo", hawezi kufanya kazi yoyote akihofia kundoka.

"Ninamshukuru Mungu baada ya matibabu niliweza kuanza kujitafuta, nikasomea mambo ya IT na sasa ninafanya kazi, nimeanza pia kuwasaidia wenye matatizo haya lengo ni kuwaelimisha waende hospitalini, ndiko kwenye matibabu sahihi," anasisitiza.

Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, alisema jana wamepanga kuwafikia wagonjwa wengi kuwapa elimu ili wapate huduma za matibabu sahihi ya hospitalini.

Alisema takwimu zinaonesha duniani watu milioni 50 wanaugua ugonjwa huo wakati nchini kuna watu kati ya 20 hadi 30 kati ya watu 1,000 na tatizo kubwa linalofanya wengi kukosa matibabu sahihi ni wengi kuendelea kuwa na imani za kishirikina.


## TANGAZO LA MNADA

Crisam,Mofano,Rapitech na Marmboto Auctioneeer Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya mnada wa hadhara wa Magari Jijini Dar es salaam na Arusha Mteja anashauriwa kulipa deni ndani ya siku 14 kutoka tarehe ya hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe ya Mnada inavyoonekana hapa chini.

| Jina la mdaiwa | DHAMANA | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| Andrew Vicent Rwechungura | Toyota Mark 11 T199DFP | 29.02.2024 |
| Aziza Issah Abdallah | Toyota Premio T153AVG | 29.02.2024 |
| Hosea Peter Magelanga | Honda stepwagon-T903EDZ | 29.02.2024 |
| Baraka Nyang'anyi Marela | Toyota passo T698 DWD | 29.02.2024 |

**Masharti ya Mnada.**

1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25% (au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%) litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

**Kwa Mawasiliano Piga 0677014355(Fanikiwa)**



**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**THE LAND ACT, 1999**
**(NO4 OF 1999)**

**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFER**

**DATE: 31/01/2024**
**REF NO: KGT/CPS/B.I/VOL.XI/12**
**APPLICANT: EMILY DASTAN NYAREMBE**
**REGISTERED OWNER: FRIDOLIN MBUNDA**
**LAND PLOT NO. 389 BLOCK 'O' LOCATION MWANGA**

Take notice that the original letter of offer of the land described above is said to be lost and I intend to issue a certified copy of the original letter of offer in Liue thereof causes to the contrary is shown within one month from the date of this publication.

The original Letter of Offer if found, should be returned to the Office of Municipal Director, P.O.BOX 44 Kigoma

Elias D. Mwazembe
Authorised Land Officer
Kigoma/Ujiji Municipal Council



**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT.**
**(CAP 117)**
**DEED POLL**

BY THIS DEED, I the undersigned now and latterly called PATRICIA SELESTINE MASERANGO DO HEREABY absolutely renounces and abandon the use of my former names PATRICIA MALEKELA KIMATA as appeared in Public Service social security fund (PSSF) with registration No. 839069 and in lieu thereof do assume from the date hereof my name of PATRICIA SELESTIN MASEGARO as appeared in my National card with Entry No 19600812 47102 0000119.
And in pursuance of such change of my names as aforesaid I HEREBY DECLARE that, I shall at all times hereafter in all records, deeds, instruction, instrument in writing in all actions and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever use and sign the said name of PATRICIA SELESTIN MASEGARO so renounced as aforesaid.
AND I HEREBY authorize and request all persons to designated and address me by such assumed name PATRICIA SELESTIN MASERAGO as appeared in my National Identity card with Entry No 19600812471020000119
IN A WITNESS WHEREOF I have hereunder signed my assumed name of PATRICIA SELESTIN MASERAGO and I have set my hand this 9 day of February, 2024.

Signed and Delivered at Kigoma
By the said PATRICIA SELESTIN MASERAGO who is
Introduced to me by ...........................or
Who is personally known to me in my presence
This 30 day of January, 2024.

DEPONENT



BEFORE ME
Name:
Qualification:
Signature:
Address:
Commissioner for oath



**DEED POLL**
**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS**
**ACT (CAP. 117)**

**T**HIS DEED is made this 25th day of January, 2024
BY THIS DEED POLL, I, MWASHABAN SULTAN PUGGA Adult, Muslim, Tanzanian Citizen of P.O.Box Dar es salaam, lately called MWASHABANI SULTAN PUGGA, MWASHABAN S. MOHAMED or MWASHABANI S. M. KOMBO. DO HEREBY absolutely renounce and abandon the use of my names namely MWASHABANI SULTAN PUGGA, MWASHABAN S. MOHAMED or MWASHABANI S.M. KOMBO appear on my Bank Account, NHIF Card No. 403701760078.3 and my NSSF Documents (CHQ No. 2929354), and in lieu thereof DO CONFIRM TO continue to use as from the date hereof the name of MWASHABAN SULTAN PUGGA only.
AND IN PURSUANCE OF SUCH REENUNCIATION of my former names of MWASHABANI SULTAN PUGGA, MWASHABAN S. MOHAMED or MWASHABANI S.M. KOMBO. I hereby declare and confirm that in all proceedings and in all such dealings or transactions whatsoever use and sign and be known by the name of MWASHABAN SULTAN PUGGA only.
AND I HEREBY authorize and request all persons to designate and address me in my name of MWASHABAN SULTAN PUGGA appear on my National Identification Card No. 19610115-15101-00001-14.
IN WITNESS WHEREOF, I have hereunder signed my name of MWASHABAN SULTAN PUGGA and have set my hand thereto in the day and the year hereinafter set forth.

SIGNED and DELIVERED By the said
MWASHABAN SULTAN PUGGA
Who is known to me personally,
This 26th day of January 2024

DEPONENT



Witnessed By:
NAME
SIGNATURE
POSTAL ADDRESS
QUALIFICATION
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO



**IN THE DISTRICT COURT OFDODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 1156 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late ISAYA MLUNGWANA SUNYAI of Dodoma Municipal - Dodoma City**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**

**BY WILLIAM NGOBITO NDYANI**

**PETITION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION WHEN DECEASED DIED INTESTATE**
**(SECTION 56)**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioner thereof.
Objections to the grant should be filed on or before the 26 th Day of FEB, 2024
**Dated at Dodoma this 23RD Day of JAN, 2024.**

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE I/C
DODOMA DISTRICT

# EU yasisitiza uhuru wa kijamii Senegal

**DAKAR, Senegal**

UMOJA wa Ulaya (EU) umesisitiza mamlaka nchini Senegal kutoa hakikisho la msingi wa uhuru wa umma baada ya machafuko yaliyosababishwa na kuahirishwa kwa uchaguzi wa rais na kugharimu maisha ya watu watatu.

Msemaji wa ofisi ya sera za mambo ya nje na usalama wa umoja huo, Nabila Massrali, kupita ukurasa wa X aliandika "Umoja wa Ulaya unatoa salamu zake za pole kwa jamaa za waliouawa na kutoa wito kwa mamlaka kuhakikisha upatikanaji wa msingi wa uhuru."

Katika hatua nyingine idadi ya waliokufa katika kipindi hiki ambacho taifa hilo limegubikwa na maandamano yaliyosababishwa na kuahirishwa kwa uchaguzi wa rais hadi Desemba imeongezeka na kufikia watu watatu.

Idadi hiyo inaelezwa katika kipindi ambacho wasiwasi ukiongezeka kwenye taifa hilo linalotazamwa kama mfano wa kidemokrasia katika eneo la Afrika Magharibi ambalo limekumbwa na tisho la matukio ya mapinduzi. Tangazo la kucheleweshwa kwa uchaguzi, ikiwa ni takriban majuma matatu kabla ya ule uliopangwa kufanyika Februari 25 umezusha vurugu za makabiliano ya polisi na raia mjini Dakar na maeneo mengine ikiwa ni nyongeza ya wimbi la maandamano ambayo inawafanya wengi wawe na hofu ya kuvurugika kwa amani katika kipindi kirefu.

Rais wa Senegal, Macky Sall, alisema kuwa kuchelewesha ni muhimu kwa sababu migogoro ya uchaguzi ilitishia uhakika wa zoezi la uchaguzi, lakini baadhi ya wabunge wa upinzani wamekosoa hatua hiyo na kusema kuwa ni mapinduzi ya kikatiba.

Wakati malalamiko ya wananchi yakiongezeka, Jumuiya ya Kiuchumi ya Mataifa ya Afrika Magharibi, (ECOWAS) na mataifa ya kigeni yalimsisitiza Rais Sall kurejea katika misingi ya kawaida ya uchaguzi.

Ndiame Diop, meneja wa hospitali ya Ziguinchor, aliliambia shirika la habari la Uingereza, Reuters, kwamba walijaribu kumwokoa kijana mmoja alipofika hospitali na kwa bahati mbaya alifariki akiwa katika chumba cha wagonjwa mahututi.

Aliongoza kuwa ilikuwa ngumu kwa mara moja kubaini kiini cha kifo chake pasipo uchuguzi wa maiti.

Wabunge wa upinzani na wagombea urais wanaokataa kuahirishwa kwa tarehe ya uchaguzi, wamewasilisha malalamiko ya kisheria na kusema watamkataa na kumtambua Sall kama rais baada ya mamlaka yake ya awali kumalizika mapema Aprili.

**DW**



Maandamano ya Senegal katika mitaa ya Dakar. Mwandamanaji akionesha ishara huku wengine wakipiga picha wakati wa makabiliano na polisi wa kutuliza ghasia. **PICHA: MTANDAO**

# Hatia uhaini kuwatia kitanzini wanajeshi DRC

**KINSHASA, DRC**

SERIKALI ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) inalengo la kurejesha adhabu ya kifo, ambayo ilisitishwa miaka 20 iliyopita, kwa wanajeshi wanaopatikana na hatia ya uhaini dhidi ya waasi wa M23.

Hiyo ni kwa mujibu wa ripoti ya baraza la mawaziri, ikielezwa kuwa hukumu za kifo hutolewa mara kwa mara na mahakama nchini DRC lakini zilibadilishwa kuwa za kifungo cha maisha gerezani tangu kuondolewa kwa hukumu ya kifo mwaka wa 2003.

Msemaji wa serikali hiyo, Patrick Muyaya, alisema Waziri wa Sheria nchini humo siku chache zilizopita aliwasilisha barua kwa baraza la mawaziri kuhusu kuondoa katazo la hukumu ya kifo kwa wanajeshi.

Pia alisema katika lengo la kukomesha uhaini, baraza la ulinzi lilimwomba Rais wa nchi hiyo, Yoweri Museven kuondoa katazo hilo kipindi hiki ambacho taifa hilo linakabiliwa na uchokozi kutoka Rwanda, ambayo inakanusha madai ya kuwasaidia waasi wa M23.

**VOA**

**Msemaji wa serikali hiyo, Patrick Muyaya, alisema Waziri wa Sheria nchini humo siku chache zilizopita aliwasilisha barua kwa baraza la mawaziri...**

# Mateka wawili wa Israel waokolewa

**JERUSALEM, Israel**

ISRAEL imesema imewaokoa mateka wawili wa kiume Fernando Marman (60) na Louis Har (70) katika mji wa kusini wa Rafah, baada ya kutekeleza shambulio katika eneo hilo lenye idadi kubwa ya wakimbizi wa kipalestina waliokimbia makazi yao kutokana na vita.

Katika taarifa ya msemaji wa Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF), Daniel Hagari, alisema vikosi vya taifa hilo vilivunja jengo katikati ya Rafah, na kufanikiwa kuwapata mateka hao kwenye ghorofa ya pili wakishikiliwa na wanachama wa Hamas wenye silaha.

Hagari alisema kwamba tangu wakati wa kuingia, askari walilinda Marman na Har kwa miili yao hadi walipofika sehemu salama, huku kukianzishwa vita na mabadilishano makali ya risasi katika maeneo kadhaa kwa wakati mmoja.

"Hii ni operesheni ambayo tumekuwa tukiitayarisha kwa muda, wawili hao walichukuliwa kutoka Nir Yitzhak kibbutz na Hamas tarehe saba Oktoba na walikuwa wameshikiliwa mateka tangu wakati huo," alisema.

Ilielezwa kuwa katika shambulio hilo la Israel lililotekelezwa asubuhi ya jana, ndege ililenga gari karibu na Hospitali ya serikali ya Bint Jbeil na kusababisha majeraha.

Pia inaelezwa kuwa Israel ilishambulia gari katika mji wa Jadra, kilomita 40 kutoka mpaka wa Israel na Lebanon, ikiwa ni shambulio la pili nje ya mpaka wa kusini tangu kuongezeka kwa vita huko Gaza. Chanzo cha usalama cha Lebanon kiliiambia Agence France Presse kwamba kiongozi wa Hamas Basil Saleh, ambaye anasimamia kitengo cha kuajiri watu katika Ukingo wa Magharibi, ndiye aliyelengwa na shambulio hilo lakini alinusurika.

Ilibainishwa kuwa Hezbollah ililenga maeneo ya kijeshi ya Israel yanayaounga mkono Gaza, huku jeshi la Israel likijibu kwa mashambulizi ya anga na mizinga, ambayo inasema inalenga miundombinu ya chama na harakati za wapiganaji karibu na mpaka.

Wizara ya Afya ambayo iko chini ya Hamas pia ilibainisha kuwa katika mashambulizi hayo kwa upande wa Rafah watu 67 wameuawa na wengine 236 wameuawa kusini mwa Lebanoni, wakiwamo wapiganaji 170 wa Hezbollah, raia 30 na waandishi wa habari watatu.

**BBC**

HABARI MICHEZO

# BIASHARA YAISHUSHA PAMBA, MKUMBUKA NYOTA YATAKATA

Na Adam Fungamwango

BAO pekee lililofungwa na straika Boban Zirintusa, liliipandisha Biashara United hadi nafasi ya pili katika mechi ya Ligi ya Championship dhidi ya Fountain Gate Talents iliyochezwa kwenye Uwanja wa Karume ulioko Musoma, mkoani Mara juzi.

Biashara United ipo katika harakati ya kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kuteremka msimu wa 2021/22, kwa sasa imefikisha pointi 46 huku vinara, KenGold wakiwa na pointi 47.

Matokeo ya wiki hii, yanaiweka Pamba FC ya Mwanza katika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 44 kibindoni.

Kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona, Mtwara wenyeji Mbeya Kwanza walipata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya TMA na kufikisha pointi zake 42, ikiwaacha wageni wao wakibaki nafasi ya tano na pointi 38.

Mechi nyingine iliyochezwa juzi ilikuwa ni kati ya Cosmopolitan iliyoichapa mabao 2-0 Mbeya City.

Wakati huo huo, straika aliyesajiliwa na Mashujaa FC kutoka Ligi ya Championship, Emmanuel Mtumbuka, kipindi cha dirisha dogo la usajili amekuwa tishio kwa kuifungia timu hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara mabao mawili kwenye mechi mbili mfululizo alizocheza. Mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu ilikuwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam akiingia kipindi cha pili wakati timu yake ikicheza dhidi ya Yanga, mpira wake kwa kwanza tu alioupata akiwa mita 20, aliachia shuti kali lililojaa wavuni na kuisawazishia timu yake bao, kabla ya Yanga kuandika goli la pili la ushindi.

Juzi, akicheza mechi yake ya pili kwenye Uwanja wa Jamhuri, Dodoma, Mtumbuka, alifunga bao dakika ya 26 kwa mtindo ule ule wa shuti kali, lakini baadaye Dodoma Jiji ilisawazisha mechi ikaisha kwa sare ya bao 1-1.

„Kuna ugumu kucheza Ligi Kuu, tofauti na Championship, na nimeuona wakati wa mechi yangu ya kwanza dhidi ya Yanga, nadhani labda kwa sababu ilikuwa ya kwanza kucheza kwenye daraja kubwa tena na timu kubwa, lakini ukweli ni huku kuna ubora wa wachezaji,“ alisema Mtumbuka.




Washindi wa Kampeni ya Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP, Otto Lwamasha (kushoto), Arnold Projectus (katikati) na Greyson Sendalo, wakifurahia zawadi walizokabidhiwa katika droo iliyofanyika wakati wakiangalia fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), kwenye viwanja vya Furahisha jijini Mwanza juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Twende Zetu AFCON yasifiwa

Na Mwandishi Wetu, MWANZA

WAKATI Ivory Coast ikitwaa ubingwa wa michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), Kampeni ya Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP iliyosimamiwa na Betika na Tigo ilihitimishwa na amsha amsha mbalimbali jijini, Mwanza juzi.

Kampeni hiyo, mbali na kutoa washindi 18 kila mmoja akiondoka na luninga ya nchi 70, dishi na dikoda ya DSTV iliyolipiwa, pia ilitoa zawadi nyingine zikiwamo fedha taslimu.

Zawadi kubwa ilikuwa ni kuwapeleka washindi sita Ivory Coast kushuhudia baadhi ya mechi ikiwamo kati ya Taifa Stars dhidi ya Morocco, mchezo wa hatua ya makundi.

Ofisa Habari wa Betika-Tanzania, Rugambwa Juvenalius, alisema droo hiyo ilitimishwa katika sherehe maalumu ambapo mashabiki waliangalia fainali ya AFCON pamoja.

„Tuliweka ‚skirini' kubwa kabisa kwenye viwanja vya Furahisha jijini Mwanza na kuungana na mashabiki wetu kushuhudia fainali hiyo katika hitimisho la droo hii iliyofanyika kwa mafanikio kwenye maeneo mbalimbali kote nchini, lengo likiwa kuwaleta mashabiki wengi kushuhudia fainali hizo pamoja,“ alisema Rugambwa.

Ofisa huyo alisema utaratibu huo ulianzia kwenye viwanja vya Tanganyika Peakers, Kawe halafu ukahamia NIT, Mabibo, Mbagala Zakheim.

Mmoja wa washindi, Otto Lwamasha, alisema ushindi umempa chachu ya kuendelea kubeti na kuongeza awali aliamini washindi wanapangwa, lakini kumbe ni tofauti na alivyokuwa akifikiria.

## Twiga Stars macho yote tiketi Olimpiki

Na Saada Akida

WACHEZAJI wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), wamewaomba Watanzania kuwapa ushirikiano na kuahidi watafanya vizuri katika mchezo wa kusaka tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki dhidi ya Afrika Kusini utakaochezwa Februari 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Fatuma Issa (Fetty Densa), alisema kikosi chao tayari kimeingia kambini na kila mchezaji yuko imara kuhakikisha anafuata maelekezo wanayopewa ili kufikia malengo ya kufanya vizuri.

Densa alisema kazi kubwa wanayokwenda kuifanya uwanjani ni kupambana kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania ili wasonge mbele katika michuano hiyo ambayo itachezwa kuanzia Julai 26 hadi Agosti 11, mwaka huu jijini Paris, Ufaransa.

"Kikubwa Watanzania waje uwanjani kutusapoti, hautakuwa mchezo rahisi lakini tutapambana na kuiheshimisha Tanzania kwa kupata matokeo mazuri nyumbani," alisema beki huyo anayeichezea Simba Queens.

Naye mshambuliaji wa timu hiyo, Aisha Mnunka, ambaye msimu huu amekuwa ‚moto' alisema sasa ni muda wao wa kupambana na kuipa Tanzania heshima kwa kupata nafasi ya kushiriki michezo ya Olimpiki ya mwaka huu.

## Meza yaota michuano Kanda ya Tano Afrika

Na Shufaa Lyimo

TANZANIA inatarajia kushiriki mashindano ya Kanda ya Tano ya mpira wa meza yatakayofanyika kuanzia Aprili Mosi, mwaka huu nchini Uganda, imeelezwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ufundi ya Chama cha Mpira wa Meza Tanzania (TTTA), Yahya Vullu, aliliambia gazeti hili maandalizi kuelekea mashindano hayo yanaendelea vyema na wachezaji wameshaingia kambini.

Vullu alisema TTTA imeandaa mashindano madogo yatakayofanyika mwezi ujao hapa jijini Dar es Salaam yenye lengo la kupata wachezaji watakaounda Timu ya Taifa itakayokwenda kupeperusha bendera ya Tanzania huko Uganda.

„Tumepata mwaliko wa kushiriki mashindano hayo ya Afrika Mashariki, kwa sasa tunapambana kuhakikisha timu yetu inakwenda huko ikiwa imara na itakayofikia malengo,“ alisema Vullu.

Mwenyekiti huyo alisema TTTA inaendelea kufanya mazungumzo na taasisi pamoja na wadau mbalimbali wa hapa nchini ili kuhakikisha fedha za kufanikisha maandalizi ya safari yao zinapatikana.

## ZISIKUPITE

### MBAPPE BADO AJIPANGA

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe, mwenye umri wa miaka 25, bado hajakubali masharti ya kujiunga na Real Madrid mara mkataba wake utakapomalizika huku klabu hiyo ya LaLiga ikihangaika kufanya mazungumzo na mama yake ambaye ni wakala wake, Fayza Lamari. **(Marca)**

### ANCELOTTI- HATUMTAKI MBAPPE

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amedokeza timu hiyo haimhitaji mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Kylian Mbappe, kwa sababu tayari wana „wachezaji sita bora duniani". **(Goal)**

### ARSENAL, CHELSEA VITANI

ARSENAL na Chelsea ni moja ya klabu zinazomnyatia winga wa Athletic Bilbao, Nico Williams, mwenye umri wa miaka 21. **(Fabrizio Romano, via Caught-Offside)**

### CAMARDA KUJIFUNGA MILAN

KINDA wa AC Milan, Francesco Camarda, atatia saini mkataba wake wa kwanza na Rossoneri hao wakati chipukizi huyo Mtaliano atakapofikisha umri wa miaka 16 mwezi ujao licha ya Manchester City na Borussia Dortmund kumtaka. **(Calciomercato, via Football Italia)**

### KELLY KUTUA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inafikiria kumsajili beki wa Bournemouth, Lloyd Kelly, mwenye umri wa miaka 25 msimu huu wa joto. **(Mail)**

### BARCA YAMTAKALIA TORRES

BARCELONA haina nia ya kumruhusu mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Hispania, Ferran Torres, mwenye umri wa miaka 23, kuhama klabu hiyo msimu wa joto. **(Mundo Deportivo)**

### MOURINHO KUMRITHI TUCHEL

JOSE Mourinho mwenye umri wa miaka 61, yuko tayari kuchukua nafasi ya kuifundisha Bayern Munich, ikiwa klabu hiyo itaamua kumfukuza, Thomas Tuchel (50). **(Bild)**

### ALEXANDER SAFI LIVERPOOL

LIVERPOOL ipo tayari kumpa mlinzi wa England, Trent Alexander-Arnold, 25, mkataba mpya wa muda mrefu. **(Football Insider)**

### ADARABIOYO ANUKIA LIVERPOOL

KLABU ya Liverpool inamfuatilia mlinzi wa Fulham, Tosin Adarabioyo, mwenye umri wa miaka 26, kwa ajili ya uhamisho unaowezekana msimu huu wa joto. **(Mail)**

### MCGUIRE ATAJWA ENGLAND

KLABU ya Sheffield Wednesday inapania kuwasilisha ofa ya kumnunua mshambuliaji wa Orlando City na Marekani, Duncan McGuire, mwenye umri wa miaka 23, ikiwa klabu hiyo haitashushwa daraja msimu huu. **(Sun)**

### YAZICI AGOMBEWA ULAYA

KIUNGO wa kati wa Uturuki na Lille, Yusuf Yazici, anawaniwa na klabu kadhaa za Ulaya, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 akielekea kuondoka Ufaransa baada ya mkataba wake wa sasa utakapokamilika msimu huu wa joto. **(Fabrizio Romano)**

## DONDOO … SOKA MAGAZET… LAYA




# HALLER AIBEBA IVORY COAST AFCON 2023

**Troost-Ekong atangazwa Mchezaji Bora, Williams, Afrika Kusini...**

**ABIDJAN, Ivory Coast**

SEBASTIEN Haller kwa mara nyingine tena alikuwa shujaa wa Ivory Coast wakati wenyeji walipotoka nyuma na kuwafunga Nigeria mabao 2-1 na kutwaa ubingwa wa michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) katika fainali iliyochezwa juzi.

Mshambuliaji huyo, ambaye alifunga bao la ushindi katika mechi ya hatua ya nusu fainali ikiwa ni miezi 13 tu tangu arejee kutoka matibabu ya saratani ya tezi dume na aliunganisha krosi ya Simon Adingra kwa mguu wa kulia zikiwa zimesalia dakika tisa kukamilisha mchezo huo na kuibua shangwe kali jijini Abidjan.

Ugonjwa huo ambao ulitishia hatima yake ya uchezaji mpira ulimfanya kukaa nje ya dimba akipata matibabu kwa zaidi ya mwaka mmoja.

William Troost-Ekong alikuwa ameiweka Nigeria mbele dakika saba kabla ya kumalizika kwa kipindi cha kwanza wakati beki huyo wa kati alipopanda juu zaidi na kufunga kwa kichwa kutoka umbali wa yadi tisa akiunganisha mpira wa kona.

Franck Kessie alifunga bao la kusawazisha dakika ya 62 baada ya kuachwa bila kuthibitiwa kwenye eneo la hatari na akapiga kichwa kutokana na mpira wa kona ya Adingra.

Baada ya kukimbia kwa kasi hadi fainali, ambayo ni pamoja na kuondoka kwa kocha Jean-Louis Gasset baada ya kushindwa mara mbili katika hatua ya makundi, Ivory Coast walinyakua taji hilo ikiwa ni mara ya tatu katika historia yao.

Wenyeji hao wa Afrika Magharibi, awali walishinda taji hilo mwaka 1992 na 2015 na kuwa waandaaji wa kwanza wa michuano hiyo kushinda tangu Misri ilipotwaa kombe hilo mwaka 2006.

Kocha wa muda, Emerse Fae, ndiye aliyeipa mafanikio Ivory Coast kupita hatua ya mtoano, ambayo ilijumuisha ushindi mnono dhidi ya mabingwa watetezi Senegal na Mali baada ya kusawazisha dakika za lala salama katika michezo yote miwili.

Ivory Coast ilitumia zaidi ya dola bilioni moja kuandaa michuano hiyo, ikiwekeza kiasi sawa na hicho katika kuboresha miundombinu nchini humo, na Rais wake, Alassane Outtara, alijiunga na sherehe za baada ya mechi katika uwanja huo uliopewa jina lake.

Ushindi huo umewafanya Tembo hao kuzawadiwa dola milioni saba, huku Nigeria ikikabidhiwa dola milioni nne na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Kwenye fainali hiyo, Adingra, mwenye umri wa miaka 22 alitwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa mechi.

Nahodha wa Nigeria, Troost-Ekong, aliondoka na tuzo ya Mchezaji Bora wa AFCON.

Mchezaji hatari wa Guinea ya Ikweta, Emilio Nsue Lopez, ameondoka na tuzo ya PUMA ya kiatu cha dhahabu kwa mabao yake matano yaliyomfanya kuwa kileleni mwa wafungaji bora wa michuano hiyo.

Golikipa wa Afrika Kusini, Ronwen Williams, alichaguliwa Kipa Bora wa michuano hiyo na mbali na kushika nafasi ya tatu katika mashindano hayo, Afrika Kusini ilitwaa tuzo ya mchezo wa kiungwana, Fair Play.

HABARI MICHEZO

# SAKA: TULINUKA DAMU NA KUDHAMIRIA 'KUUA'

**LONDON, England**

BUKAYO Saka alisema Arsenal „ilinusa damu na kutaka kuua" katika ushindi wao wa kikatili wa mabao 6-0 dhidi ya West Ham katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa kwenye Uwanja wa London Jumapili iliyopita.

Arsenal sasa wamepitwa pointi mbili wakiwa nafasi ya tatu katika msimamo baada ya mabao ya kichwa kutoka kwa mabeki wawili wa kati, William Saliba na Gabriel, Saka alifunga penalti dakika ya 41 na mkwaju mzuri wa Leandro Trossard uliwaweka mbele kwa magoli 4-0.

Maelfu ya mashabiki wa West Ham waliamua kuondoka uwanjani wakati wa mapumziko.

Wakiwa hawapo, Saka alifunga tena dakika ya 63 kabla ya Declan Rice kufyatua shuti kali la umbali wa yadi 25 na kukataa kushangilia dhidi ya timu yake ya zamani baada ya kuhamia kwa washikabunduki hao kwa uhamisho wa pauni milioni 105 msimu uliopita.



„Tulikuwa mbele kwa mabao 4-0 katika kipindi cha kwanza na tungeweza kufunga mengine mengi, ikiwa ni pamoja na mimi," alisema Saka akiiambia Sky Sports.

„Nadhani tulinuka damu leo (juzi) na kwenda kuua. Tulifanya vizuri sana kufunga zaidi na tulifurahi sana."

Huo ulikuwa ni ushindi wao mkubwa zaidi kuwahi kutokea ugenini katika historia ya Ligi Kuu England.

Alipoulizwa kama maoni ya Saka yalikuwa ni dalili ya timu iliyo tayari kuwawinda wapinzani wao wa ubingwa, Arteta aliongeza : „Ninachonusa ni timu ambayo inataka kuwa bora na bora. Jinsi walivyofanya mazoezi wiki hii, walikuwa na umakini kabisa.

„Tunadumisha na kuongeza kasi sasa na uchezaji, wamekuwa na nguvu na matokeo na tunahitaji kudumisha hilo kwa sababu sio sisi pekee.

„Tunajua viwango na kiwango tunachokabiliana nacho na tunahitaji kuwa katika kiwango hiki ikiwa tuna nafasi yoyote ya kufanikiwa."

## Xavi: Barca bado iko ‚vitani' Laliga

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernández alikataa kurusha taulo kwenye LaLiga licha ya sare ya 3-3 Jumapili dhidi ya Granada na kuifanya timu yake kuachwa pointi 10 na vinara wa ligi hiyo, Real Madrid.

Lamine Yamal alifunga bao la kuongoza kwenye Uwanja wa Olimpiki, lakini katika mchezo mwingine uliowekwa alama na ulinzi wa kuchekesha, Barca walijikuta wakiwa chini 2-1 na 3-2 dhidi ya Granada.

Bao la pili la Yamal usiku huo liliipatia Barca pointi lakini mabao mawili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 16 hayakuzuia timu hiyo ya Katalunya kuangusha pointi mbili zaidi kwenye mbio za ubingwa.

„LaLiga tayari ilikuwa ngumu na sasa inazidi kuwa ngumu zaidi na pointi nyingi zimepotea," alisema Xavi katika mkutano wa waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

„Ni pengo kubwa kwa Madrid na tano sasa kwa Girona (iliyo nafasi ya pili), lakini hatutatupia taulo.

„Tunachotakiwa kufanya sio kuteleza tena. Tulipata nafasi za kuua mchezo na nadhani tumewapa Granada mabao wakati kulikuwa na hatari ndogo. Timu ilikuwa na imani, ujasiri na nia, lakini haikutosha, hufanya mambo kuwa magumu zaidi."

Msimu wa Barca umechangiwa na ulinzi mbaya, Ricard Sánchez na Facundo Pellestri waliwapa Granada mabao ya kuongoza, huku Robert Lewandowski akisawazisha kabla ya Ignasi Miquel kurejesha faida ya mgeni.

Hii ilikuwa mara ya pili ndani ya mwezi mmoja kwa Blaugrana hao kufunga mabao matatu wakiwa nyumbani na kushindwa kushinda baada ya kufungwa 5-3 na Villarreal Januari.

Sasa wameruhusu mabao 24 katika michezo 11 katika michuano yote mwaka 2024, zaidi ya timu nyingine yoyote kwenye ligi tano bora za Ulaya.

„Tulijitolea sana kwa kujilinda," aliongeza Xavi.

„Tuliruhusu mabao matatu dhidi ya Villarreal; kisha tena leo (juzi). Hiyo inafanya kuwa vigumu kushinda chochote.

„Lazima tupunguze makosa. Ni makosa yale yale katika safu ya ulinzi ambayo yameonyesha msimu huu. Ilikuwa vivyo hivyo kwenye sare ya Granada mapema kwenye kampeni."

Nguvu ya Barca waliposhinda taji msimu uliopita ilikuwa ni ngome yao. Baada ya mechi 24 za ligi, walikuwa wamefungwa mara nane pekee, hatua sawa ya kampeni hii.

„Ni mchezo," alisema Xavi alipoulizwa kushughulikia tofauti hiyo. "Mabadiliko ya kiwango, kupoteza wachezaji ambao hawajaweza kucheza pamoja... makosa ya umakini.

„Tumefanya mambo mengi mazuri kushinda michezo mingi, lakini makosa haya kwenye safu ya ulinzi ndio tofauti ya pointi kati yetu na Madrid na Girona."

Baada ya kushindwa kwa Villarreal, Xavi alitangaza kujiuzulu mwishoni mwa msimu huu.

Alisema matokeo ya Granada ni „kurudi nyuma" lakini akapendekeza kukimbia kwa pointi saba kutoka tisa tangu uamuzi wake ulionyesha kumekuwa na majibu kutoka kwa wachezaji wake.

## McTominay amkosha Ten Hag

**MANCHESTER, England**

ERIK ten Hag alimsifu, Scott McTominay, kama mfano wa kuigwa kwa wengine baada ya nyota huyo kutoka benchi na kuipa ushindi wa Manchester United dhidi ya Aston Villa inayowania kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Pambano la Jumapili kati ya timu hizo zinazoshika nafasi ya tano na sita kwenye dimba la Villa Park lilianza huku Rasmus Hojlund akifunga bao katika mechi yake ya tano mfululizo ya Ligi Kuu England.

United walipoteza njia baada ya bao la kwanza la dakika ya 17 katika mwanzo mzuri na hatimaye Villa wakapata goli lililostahili kipindi cha pili kupitia kwa Douglas Luiz.

Lakini Mashetani Wekundu walijichimbia na McTominay akafanya matokeo kuwa 2-1 dakika ya 86 baada ya kukutana na krosi ya Diogo Dalot kwa kichwa - bao lake la nne la Ligi Kuu England msimu huu akitokea benchi.



Ten Hag alisema kuhusu mchezaji ambaye jumla ya mabao yake katika Ligi Kuu England msimu huu ni saba: „Nadhani yeye ni mfano kwa wachezaji wengine wengi siku hizi.

„Hakuna wachezaji wengi ambao wanaweza kutoka kwenye benchi na kuleta nguvu hii, yuko tayari kwa kila dakika, akichangia timu kila wakati. Mpira ni mchezo wa timu na tunasahau mara nyingi.

„Lakini Scott ndiye mfano, kila wakati akitoa roho, katika juma anapofanya mazoezi, akifanya mambo sahihi, akijishughulisha mwenyewe.

„Yupo tayari kwa dakika moja, yuko tayari kwa dakika 90, yuko tayari kila wakati. Nadhani ni vizuri kuwa na mchezaji wa aina hiyo."

HABARI MICHEZO

# SIMBA YAENDELEA KUITESA AZAM IKIWAZA POINTI TISA

**Na Saada Akida**

HUKU bado akiwaza sare dhidi ya Simba, Kocha Mkuu wa Azam FC, Youssouph Dabo, amesema timu yake ina 'kibarua kigumu' cha kuhakikisha inavuna pointi tisa mwezi huu ili kujiimarisha kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea, imefahamika.

Azam FC iliamini itaondoka na pointi tatu lakini Simba ilifanikiwa kupata bao la kusawazisha katika dakika za lala salama kupitia kiungo wake Mzambia, Clatous Chama.

Dabo ameliambia Nipashe anataka kuona Azam FC inaondoka na pointi tisa kutoka kwenye mechi tatu zinazofuata ili kuendelea na kampeni ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu. Kocha huyo alisema wamerudi kwenye uwanja wa mazoezi kusahihisha makosa yao na sasa wanaendelea na mikakati kuhakikisha wanapata matokeo mazuri watakapoivaa Geita Gold FC.

"Malengo yetu ni kuvuna alama tatu katika kila mechi, kwa mwezi (Februari) huu tulihitaji pointi 12, lakini tumepoteza mbili kwa Simba, bado mechi tatu, moja nyumbani na mbili ugenini, hizo zote tunahitaji pointi tisa muhimu ili kutuweka katika nafasi nzuri kufikia malengo yetu," alisema kocha huyo.

Aliongeza ligi imekuwa na ushindani kwa sababu kila timu imejipanga kuondoka na matokeo chanya na hatimaye kufikia malengo ya kuwania ubingwa au kujinasua na hatari ya kushuka daraja.

Azam FC inatarajiwa kuwakaribisha Geita Gold Ijumaa kwenye Uwanja wa Azam Complex halafu watasafiri kuelekea jijini Mbeya kuwafuata Maafande wa Tanzania Prisons katika mchezo mwingine wa ligi hiyo utakaochezwa Februari 25, mwaka huu.

Baada ya hapo watawafuata Singida Fountain Gate katika mechi itakayochezwa Februari 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza.

Mabingwa watetezi, Yanga wenye pointi 40 wanaongoza katika msimamo wa ligi hiyo wakifuatiwa na Azam FC yenye pointi 32 huku Simba yenye mechi pungufu ikiwa ya tatu na pointi zake 30 kibindoni.




Muuguzi wa Manispaa ya Kibiti, Halima Kituu (kulia), akimpatia ushauri wa chanjo mbalimbali na elimu ya afya mkazi wa wilaya hiyo wakati wananchi wakiangalia pamoja fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) kwenye eneo maalumu lililoandaliwa mkoani Pwani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# USAID yaandaa 'darasa' AFCON

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Maendeleo la Kimataifa la Marekani (USAID), kupitia mradi wa Breakthrough ACTION wameungana na serikali kutumia michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), ili kuendesha matamasha ya jamii yatakayolenga kuongeza msisimko wa michezo.

USAID kupitia mradi huo inafanya kazi kwa ukaribu na Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais - Utawala wa Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na MultiChoice Tanzania.

Baada ya mafanikio ya tukio la kwanza lililofanyika Temeke jijini Dar es Salaam wakati wa mchezo kati ya Taifa Stars dhidi ya Morocco, kumefanyika tukio la pili la kuangalia michezo katika ngazi ya jamii kwenye Wilaya ya Kibiti, mkoani Pwani.

Washiriki walipata huduma ikiwamo chanjo na kuimarisha kinga dhidi ya COVID-19, chanjo za kawaida za kinga, uchunguzi wa afya pamoja na ushauri wa VVU, upimaji na huduma za kuzuia VVU.

Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Kanali Joseph Kolombo alisema: "Ushirikiano kati ya USAID na Serikali ya Tanzania unadhihirisha nguvu ya ushirikiano katika kuendeleza miradi ya afya ya umma."

Alisema ushirikiano na USAID Breakthrough ACTION kupitia kampeni ya ‚Timu Chanjwa' ni uthibitisho wa dhamira ya serikali na wadau kwa pamoja kuhakikisha jamii inpata chanjo na kuimarisha mikakati ya kinga.

Naye Craig Hart, Mkurugenzi wa USAID Mission alisema: "Ushirikiano huu unathibitisha dhamira yetu ya kuendeleza afya ya umma na kujenga jamii imara. Kwa kutumia msisimko wa AFCON, lengo letu ni kutoa athari ya kudumu kwenye uelewa wa afya na huduma. Pamoja na washirika wetu, tunajivunia kuwa waanzilishi wa jitihada hii ya kubadilisha inayolingana na misheni yetu ya kuboresha ustawi wa watu nchini Tanzania."

## Kocha Prisons alia walikosa bahati

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Prisons, Hamad Ally, amesema timu yake ilikosa bahati na hivyo kusababisha kupoteza mechi dhidi ya mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya juzi.

Prisons ilichapwa mabao 2-1, na kuifanya Yanga imalize mzunguko wa kwanza ikiwa kileleni na pointi zake 40.

Akizungumza na Nipashe jana, Hamad alisema Yanga ni timu inayofanya vizuri katika michezo yake na inapata matokeo chanya kutokana na aina ya wachezaji waliokuwa nao.

Kocha huyo alisema timu yake haikuwa na kiwango kizuri katika kipindi cha kwanza na hali hiyo iliwapa nafasi wapinzani kutawala mchezo.

„Lengo langu lilikuwa ni kupata pointi tatu katika mchezo huo isipokuwa bahati haikuwa ya kwao, ninaahidi kujipanga kwa ajili ya mchezo ujao, sasa tunaelekeza nguvu zetu kuwakabili Singida Fountain Gate. Tutajipanga kuhakikisha haturudii makosa," alisema kocha huyo.

## Dawda ajitosa kuimba, chapa LPME yambeba

**Na Sabato Kasika**

MWANDISHI wa muziki nchini Gambia, Dawda, amejitosa katika uimbaji na sasa amechukuliwa na kampuni ya usimamizi wa muziki ya Falme za Kiarabu iitwayo LPME Group.

Katika kazi yake ya uandishi wa tungo za muziki amewahi kuwaandikia wasanii mbalimbali wakubwa kama Sean Kingston, Mohombi, Bayanni, Singah, Lyaz, Charice na Ashley Tisdale.

LPME inachukua wasanii wanaotokea katika utamaduni tofauti duniani, ikiangazia pia Afrika, akiwamo Dawda na wengine kutoka Senegal, Amapiano wa Afrika Kusini na miondoko ya Afro Beats ya Nigeria.

Mwandishi huyo amenukuliwa na kampuni hiyo akisema: "Nimekua nikiandika na kutayarisha nyimbo za sehemu nyingi duniani kote, hivyo nilipoamua kuanza kuimba nimetaka nionyeshe jinsi gani ninajivunia Uafrika wangu, nina furaha kuwa mbunifu katika kuunganisha kile nilichonacho ndani ya muziki nitakaotoa," alisema Dawda.

Msanii huyo tayari ameshaandaa wimbo wake wa kwanza uitwao ‚Wine' ambao ulizinduliwa Februari 8, mwaka huu na kuongeza hatua hiyo inaashiria mwanga kwa wasanii wa Afrika kupata nafasi ya kuonekana na kampuni za kimataifa.

**Michezo**

Jumanne Februari 13, 2024

Nipashe

**Haller aibeba Ivory Coast AFCON 2023** UKURASA 21






Mabingwa wa michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023), Ivory Coast baada ya kuwafunga Nigeria mabao 2-1 katika mechi ya fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Olympique Alassane Ouattara jijini Abidjan, juzi usiku. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YATETEMA MWANZA

## Ni bao pekee la Babakar Sarr, yasogea nafasi ya pili...

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mkabaji, Babakar Sarr, alifunga bao dakika tisa kabla mechi kumalizika na kuipa Simba ushindi wa goli 1-0 dhidi ya Geita Gold FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza jana.

Sarr, aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Sadio Kanoute, alipachika bao hilo kwa mguu wa kushoto akiunganisha mpira wa kichwa kutoka kwa Kibu Denis aliyekuwa kwenye kiwango cha hali ya juu jana na kuihenyesha ngome ya Geita Gold.

Sarr aliyesajiliwa na Simba kipindi cha dirisha dogo akitokea US Monastir ya Tunisia, anakamilisha idadi ya wachezaji wote wa timu ya kigeni waliosajiliwa kwenye uhamisho huo kufunga mabao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wachezaji wengine, Freddy Michael na Pa Omari Jobe, walifunga mabao yao ya kwanza katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Tabora United iliyochezwa Jumanne iliyopita kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora na kuwafanya Wekundu wa Msimbazi kuondoka na ushindi mnono wa mabao 4-0.

Bao la jana lilitengenezwa kuanzia nyuma, ambapo ulipigwa mpira mrefu na Kennedy Wilson na kumkuta mchezaji mwingine aliyeingia kipindi cha pili, Luis Miquissone, ambaye naye alianzia benchi na kuchukua nafasi ya Clatous Chama.

Baada ya Miquissone kuwalamba chenga ya kuzunguka wachezaji kadhaa wa Geita Gold alipiga krosi ambayo ilimkuta Kibu aliyeruka na kumdondoshea mfungaji kwa kichwa na bila ajizi akaukwamisha wavuni, kipa Constantine Malimi, akiwa hana la kufanya.

Matokeo hayo yanaifanya Simba kupanda hadi nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikifikisha pointi 33 na kuishusha Azam FC ambayo ina pointi 32, huku kila timu ikiwa imecheza michezo 14 mpaka sasa.

Mechi ilianza kwa Simba kufanya mashambulizi mfululizo katika lango la wenyeji wao na kama wachezaji wake wangekuwa makini wangepata mabao mawili ya mapema.

Ilikuwa ni dakika ya tatu wakati kona ya Chama ilipounganishwa na Kibu na mpira kuonekana unatinga wavuni lakini kabla haujavuka mstari, beki wa Geita Gold, Mwaita Gereza, alifanya kazi ya ziada na kuokoa hatari hiyo.

Baada ya kuokolewa ulivuka nje kidogo ya eneo la hatari ambapo ulimkuta Kanoute akiwa katika nafasi nzuri kabisa, lakini shuti alilopiga lilipaa juu huku dakika tano baadaye, Kanoute alikosa tena bao la wazi, baada ya mpira wa faulo iliyopigwa na Chama kutoka nje kidogo ya lango la Geita Gold.

Simba iliendelea na mlolongo wa kukosa mabao, safari hii ilikuwa zamu ya Shomari Kapombe, dakika ya 32 akiupata mpira nje kidogo ya eneo la 18 aliachia shuti kali, lakini liliishia katika mikono ya Malimi.

Baada ya kosakosa nyingi, Geita Gold ilionekana kuizoea Simba na sasa wakaanza kutoka nyuma na kushambulia ambapo dakika za mwisho wa kipindi cha kwanza.

Na nusura ipate bao dakika ya 44, baada ya kazi kubwa iliyofanywa na Edmund John alipoupata mpira wingi ya kushoto, akageuka na kumpenyezea Jonathan Ulaya aliyepiga shuti la chinichini lakini Aishi Manula alikuwa makini akaudaka mpira huo.

Kama ilivyotegewa, kipindi cha pili, Geita Gold walionekana kuwazoea Simba na sasa walianza kusukuma mashambulizi na kuwaweka kwenye hali ngumu mabeki wa timu hiyo wakiongozwa na Fondoh Che Malone na Kennedy Juma.

Yalikuwa ni mabadiliko la Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, kuwatoa Chama, Kanoute na Jobe na nafasi zao kuchukuliwa na Fred, Miquissone na Sarr, ndiyo yaliyobadilisha kicheko kwa Wekundu wa Msimbazi.

Baada ya kufungwa bao hilo, Geita Gold waliamka tena na kufanya mashambulizi ya mara kwa mara, dakika za majeruhi kupitia kwa Nasoro Saadun na Erick Mwijage, lakini mipira yao ilitoka juu ya lango na kuwaweka salama Simba.

Geita Gold imeendelea kubakia na pointi 19, ikiwa katika nafasi ya 10 baada ya kucheza mechi 14 mpaka sasa.

# Gamondi alikubali gwaride la TZ Prisons

**Na Saada Akida**

LICHA ya timu yake kupata ushindi wa mabao 2-1, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema haikuwa kazi rahisi kuondoka na pointi tatu katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Prisons iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya juzi.

Gamondi alisema kikubwa amefurahi kupata pointi tatu na kuendelea kujiimarisha katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha huyo alisema bado ana kazi ya kufanya katika kuiboresha safu yake ya ulinzi kutokana na kuruhusu mabao mawili katika michezo miwili iliyopita.

Alisema anafuraha kubwa ya kupata alama tatu muhimu kulingana na wapinzani wao kuwaonyesha ushindani mkubwa, hasa kipindi cha pili kuwapa nafasi ya kucheza.

"Kupata pointi tatu ni muhimu sana licha ya kucheza kwa presha kubwa, kipindi cha kwanza tulicheza vizuri na tulitengeneza nafasi na kuzitumia mbili, lakini wapinzani walipata bao moja. Kipindi cha pili hatukucheza vizuri," alisema Gamondi.

Aliongeza ataendelea kuwapa mbinu wachezaji wake ili kutorudia makosa kwa kutoruhusu nyavu zao kutingishwa kwa sababu wanahitaji kufikia malengo.

„Ninataka kuona makosa yote tunayafanyia kazi na kuwataka wawe makini ili mechi ijayo tufanikiwe kuvuna alama tatu na kutoruhusu nyavu kutikiswa," Gamondi alisema.

Naye nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, alisema kadi nyekundu aliyoonyesha kipa wao, Metacha Mnata, iliwaathiri na kusababisha kubadilisha mfumo ikiwa ni kabla ya wapinzani wao pia kupewa kadi nyekundu.

"Kipindi cha kwanza kilikuwa kizuri sana kwetu, tulitengeneza nafasi nne na kufanikiwa kupata mabao mawili, kipindi cha pili tulifanya makosa na kuruhusu kufungwa bao moja. Kwa sasa tuna changamoto ya majeraha kwa mabeki hali hiyo inapelekea kocha kufanya mabadiliko katika nafasi hiyo," alisema Mwamnyeto.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >